JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HOTUBA YA MHESHIMIWA ANTHONY PETER MAVUNDE (MB.), WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027




**DODOMA,** **APRILI, 2026**




**Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini akitazama namna ya uthaminishaji madini ya spinel katika soko la madini Mahenge, Wilaya ya Ulanga Mkoani Morogoro.**





## VIONGOZI WA WIZARA



**Mhe. Anthony Peter Mavunde (Mb.)**
Waziri wa Madini



**Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa (Mb.)**
Naibu Waziri wa Madini



**Eng. Yahya Ismail Samamba**
Katibu Mkuu



**Bw. Msafiri Lameck Mbibo**
Naibu Katibu Mkuu



## YALIYOMO


A. UTANGULIZI……… 1

B. MWENENDO WA BIASHARA YA MADINI DUNIANI 14

C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 16

(I) MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI 16
(II) FEDHA ZILIZOPOKELEWA NA KUTUMIKA 17
(III) UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 18
(IV) UTEKELEZAJI WA MAENEO MENGINE YA WIZARA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 38
(V) UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 45
a. TUME YA MADINI 45
b. TAASISI YA JIOLOJIA NA UTAFITI WA MADINI TANZANIA (GST) 55
c. SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA (STAMICO) 60
d. KITUO CHA JEMOLOJIA TANZANIA (TGC) 71
e. TAASISI YA UHAMASISHAJI UWAZI NA UWAJIBIKAJI KATIKA RASILIMALI MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA (TEITI) 74

D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 79

I. Vipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 79
II. Maeneo Mengine Yatakayotekelezwa na Wizara katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 88
III. Kazi Zitakazotekelezwa na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 93

E. SHUKRANI 111

F. HITIMISHO 113

## ORODHA YA PICHA


| Na. | Maelezo ya Picha | Ukurasa |
| --- | --- | --- |
| 1. | Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini katika kutekeleza sehemu ya majukumu yake ikikagua mtambo wa uchenjuaji wa Madini ya Dhahabu katika Kituo cha Mfano cha Lwamgasa – Geita. | 5 |
| 2. | Mheshimiwa Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini akisaini kwa niaba ya Serikali mkataba wa uchimbaji mkubwa wa madini ya Niobium utakaomilikiwa kwa ubia baina ya Serikali na Kampuni ya Panda Hill Tanzania Limited. | 12 |
| 3. | Mheshimiwa Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini (katikati) katika picha ya pamoja na wawakilishi wa kampuni ya kimataifa ya uchimbaji madini ya dhahabu ya barrick baada ya Mkutano wa Kimataifa wa “African Mining Indaba”. Upande wa kulia ni Bw. Msafiri Mbibo. Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Madini, wa pili kulia ni Mheshimiwa CPA. Simon Songe (Mb.), Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na upande wa kushoto ni Dkt. Venance Mwasse, Mkurugenzi Mtendaji STAMICO. | 25 |
| 4. | Mheshimiwa Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini akizindua mradi wa utafiti wa kina wa madini kwa kurusha helikopta unaotekelezwa na Kampuni ya Barrick. | 32 |
| 5. | Mheshimiwa Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini akishuhudia utiaji saini wa makubaliano maalum ya kuwakopesha wachimbaji wadogo kati ya Tume ya Madini na Benki ya CRDB. | 35 |
| 6. | Magari mapya manne (4) kwa ajili ya kuimarisha shughuli za utafiti GST. | 37 |

| Na. | Maelezo ya Picha | Ukurasa |
|---|---|---|
| 7. | Maafisa wakikagua masuala ya Usalama, Afya na Mazingira katika mgodi wa chini ya ardhi wa Polygold Co. LTD uliopo Musoma, Mara. | 49 |
| 8. | Kiwanda cha kuzalisha nishati safi ya Rafiki Briquettes Mkoani Tabora ambacho kilizinduliwa tarehe 21 February 2026. | 62 |
| 9. | Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa (Mb.), Naibu Waziri wa Madini akishuhudia utiaji saini wa mkataba kati ya STAMICO na Kampuni ya "Plantcor Mining and Plant Hire (PTY) Ltd" kwa ajili ya uendelezaji wa leseni za shirika katika eneo la Kigosi. | 65 |
| 10. | Kituo cha mauzo na maonesho ya madini ya vito na bidhaa za usonara kilichopo katika Ukumbi wa Mkutano wa AICC. | 74 |
| 11. | Bi. Mariam Mgaya, Katibu Mtendaji wa TEITI (wa pili kulia) akiuelimisha Umma kuhusu majukumu ya TEITI kupitia kipindi cha "Morning Trumpet", Azam TV. | 77 |

## ORODHA YA MAJEDWALI


| Na. | Maelezo ya Jedwali | Ukurasa |
|---|---|---|
| 1. | Makusanyo Halisi ya Maduhuli kwa Kila Ofisi ya RMO Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Pamoja na Makadirio Kwa Mwaka 2026/2027 | 115 |
| 2. | Kiasi cha Mrabaha na Ada ya Ukaguzi Kilichokusanywa Kutoka Kwenye Mauzo ya Madini Mbalimbali Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 | 116 |
| 3. | Mwenendo wa Mauzo na Mapato ya Dhahabu Katika Masoko ya Geita, Kahama na Chunya kwa Kipindi cha Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 | 117 |
| 4. | Mapato Yaliyotokana na Mauzo ya Madini Kwenye Masoko ya Madini Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 | 118 |
| 5. | Mapato Yaliyotokana na Mauzo ya Madini Kwenye Masoko ya Madini Kwa Kila Aina ya Madini Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 | 120 |
| 6. | Mapato Yaliyotokana na Mauzo ya Madini Kwenye Masoko ya Madini Tangu Kuanzishwa Kwake Machi, 2019 hadi Machi, 2026 | 121 |
| 7. | Makusanyo ya Maduhuli Yaliyotokana na Vyanzo Mbalimbali Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 | 122 |
| 8. | Migodi ya Uchimbaji wa Kati na Mkubwa wa Madini iliyokaguliwa Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 | 123 |
| 9. | Matukio ya Matetemeko Makubwa ya Ardhi yaliyotokea nchini Tanzania katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 | 126 |

## ORODHA YA VIELELEZO


| Na. | Aina ya Kielelezo | Ukurasa |
|---|---|---|
| 1. | Makusanyo ya Maduhuli Kutokana na Mauzo ya Dhahabu Katika Masoko Makubwa Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 | 127 |
| 2. | Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli Kuanzia Mwaka 2021/2022 hadi 2024/2025 | 127 |

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ADPA | African Diamond Producers Association |
| AGF | Arusha Gem Fair |
| AICC | Arusha International Conference Centre |
| BBC | British Broadcasting Corporation |
| BLs | Broker Licenses |
| CHAMMATA | Chama Cha Mabroka wa Madini Tanzania |
| CIL | Carbon In Leach |
| CIP | Carbon In Pulp |
| CSR | Corporate Social Responsibility |
| Dkt. | Daktari |
| DLs | Dealers Licenses |
| DMCC | District Mine Closure Committee |
| DW | Deutsche Welle |
| EDR-MIS | Extractive Data Reporting Management Information System |
| EITI | Extractive Industries Tranparency Initiative |
| ESG | Environmental Social Governance |
| FEMATA | Federation of Miners Associations of Tanzania |
| FYDP IV | The Fourth Five Year Development Plan |
| GGM | Geita Gold Mine |
| GST | Geological Survey of Tanzania |
| HIV | Human Immunodeficiency Virus |
| IAI | Investment Attractiveness Index |
| ICGLR | The International Conference on the Great Lakes Region |
| KCB | Kenya Commercial Bank |
| LBMA | London Bullion Market Association |
| LTPP | Long Term Perspective Plan |
| Mb. | Mbunge |
| MBT | Mining for a Brighter Tommorrow |
| MLs | Mining Licenses |
| MOU | Memorundum of Understanding |
| MROs | Mining Resident Offices |
| MSEAP | Mineral Sector Environmental Action Plan |
| MSMIS | Mineral Sector Management Information System |

| | |
|---|---|
| NACTVET | The National Council for Technical and Vocational Education and Training |
| NBC | National Bank of Commerce |
| NEAP | National Environmental Action Plan |
| NTA | National Technical Awards |
| PCLs | Processing Licences |
| PDAC | Prospectors and Developers Association of Canada |
| PLs | Prospecting Licenses |
| PMLs | Primary Mining Licenses |
| QDS | Quarter Degree Sheet |
| REE | Rare Earth Elements |
| RMO | Resident Mines Officer |
| SADCAS | Southern African Development Community Accreditation Services |
| SEA | Strategic Environmental Assessment |
| SML | Special Mining Licence |
| STAMICO | State Mining Corporation |
| TAMIDA | Tanzania Mineral Dealers Association |
| TAMISA | Tanzania Mining Industry Suppliers Association |
| TAWOMA | Tanzania Women Miners Association |
| TEITI | Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative |
| TGC | Tanzania Gemmological Centre |
| TMX | Tanzania Mercantile Exchange |
| TRT | Turkish Radio and Television Corporation |
| TSF | Tailing Storage Facility |
| TWIMI | Tanzania Women Miners Association |
| UAUR | United African University of Rwanda |
| VETA | Vocational Education and Training Authority |
| VOA | Voice of America |
| WIMA | Women In Mining Association |
| WRD | Waste Rock Dump |
| XRF | X-ray Fluorescence |
| ZBC | Zanzibar Broadcasting Corporation |
| ZIMEC | Zambia International Mining and Energy Conference |

## HOTUBA YA MHESHIMIWA ANTHONY PETER MAVUNDE (MB.), WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochambua bajeti ya Wizara ya Madini, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kuijalia nchi yetu amani na baraka na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki Mkutano huu wa Tatu (3). Tunamuomba aendelee kutujalia rehema, hekima, busara na umoja katika kujadili hotuba za Wizara mbalimbali ikiwemo Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka

wa Fedha 2026/2027 kwa nia ya kuendeleza Taifa letu na kuboresha ustawi na maendeleo ya Watanzania.

***3. Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake wenye maono mapana, mahiri, weledi na dhamira thabiti ya kuwaletea watanzania maendeleo jumuishi. Kwa wakati wote Mheshimiwa Rais ameendelea kuhimiza amani, uwajibikaji, utawala bora, umoja na mshikamano wa Kitaifa.

***4. Mheshimiwa Spika,*** napenda kumpongeza na kumshukuru **Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuimarisha na kulinda muungano, kusimamia masuala ya mazingira na usimamizi bora wa rasilimali zetu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

***5. Mheshimiwa Spika,*** nimpongeze pia **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuiongoza Zanzibar vizuri. Hakika kiongozi huyu amekuwa nguzo imara katika kudumisha muungano. Vilevile, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba** kwa

kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuendelea kuisimamia vyema Serikali.

***6. Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia Sekta ya Madini.

***"Ni ahadi yangu kwake na kwa Bunge lako Tukufu pamoja na watanzania kwamba nitaendelea kuitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na kwa uwezo wangu wote ili kuendeleza sekta hii muhimu"***

***7. Mheshimiwa Spika***, napongeza hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu inayotoa mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za Serikali ambayo imeonesha mafanikio ya uendeshaji wa shughuli za Serikali katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026, utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 pamoja na mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

***8. Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania. Kutokana na uzoefu na umahiri wako katika shughuli za Bunge tunaamini utalifanya Bunge kuendelea kuwa chombo imara, madhubuti na chenye kuaminika.

***9. Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kumpongeza **Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.)** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu Tukufu. Aidha, niwapongeze Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kushirikiana nawe katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa weledi mkubwa. Ni matarajio yetu kuwa chini ya uongozi wako, Bunge litaendelea kufanya maamuzi sahihi na yenye manufaa kwa maendeleo ya Taifa letu na kufanya liendelee kuheshimika ndani na nje ya nchi yetu.

***10. Mheshimiwa Spika,*** naomba niwapongeze sana **Mheshimiwa CPA. Subira Khamis Mgalu (Mb.)**, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na **Mheshimiwa CPA. Simon Songe Lusengekile (Mb.)**, Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kuteuliwa kuiongoza Kamati hii. Aidha, nawapongeza wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kuteuliwa kutekeleza majukumu ya Kamati. Wizara inaishukuru Kamati kwa ushauri wake makini ambao imekuwa ikiutoa katika kuhakikisha kuwa sekta hii inakuwa na tija kwa Taifa na kuwanufaisha watanzania. Vilevile, ninaishukuru Kamati kwa kujadili kwa kina

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 na kuyapitisha kwa kauli moja.



**Picha Na. 1:** *Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini katika kutekeleza sehemu ya majukumu yake ikikagua mtambo wa uchenjuaji wa Madini ya Dhahabu katika Kituo cha Mfano cha Lwamgasa – Geita.*

**11. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la 13 kwa kuwa sehemu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niombe ushirikiano wao katika kuendeleza sekta hii muhimu katika kujenga uchumi imara na maendeleo endelevu ya Taifa letu.

***12. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Pia, niwapongeze viongozi wote waandamizi wa Serikali walioaminiwa na kuteuliwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nyadhifa mbalimbali, nawatakia utendaji mwema katika kutekeleza majukumu yao.

***13. Mheshimiwa Spika***, kwa heshima kubwa, nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Mtumba kwa kuniamini na kunichagua. Naamini mtaendelea kushirikiana nami katika kutekeleza majukumu yangu kama mwakilishi wenu katika Bunge hili Tukufu.

"***Nawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote na kwa kipaji nilichojaliwa na Mwenyezi Mungu katika kuleta maendeleo ya jimbo na Taifa kwa ujumla"***

***14. Mheshimiwa Spika,*** napenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa (Mb.)**, kwa kuteuliwa tena na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Naibu Waziri wa Madini. Aidha, namshukuru kwa dhati kabisa kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza

majukumu ya Wizara. Hakika amekuwa ni msaada mkubwa kwangu katika kuhakikisha sekta hii inatimiza malengo yake.

***15. Mheshimiwa Spika,*** napenda kumshukuru **Eng. Yahya Ismail Samamba**, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini kwa kuratibu na kusimamia utendaji wa Wizara. Pia, nampongeza **Bw. Msafiri Lameck Mbibo**, Naibu Katibu Mkuu kwa kuendelea kumpatia ushirikiano Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini. Vilevile, nimshukuru **Dkt. AbdulRahman Shabani Mwanga**, Kamishna wa Madini kwa kutekeleza majukumu yake vizuri. Halikadhalika, nichukue fursa hii kuishukuru Menejimenti ya Wizara pamoja na wafanyakazi wote kwa ushirikiano na utendaji kazi mzuri katika kutekeleza majukumu yao.

***16. Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru Wenyeviti wa Bodi kwa ushauri na utendaji kazi kwa ufanisi katika kusimamia Sekta ya Madini. Viongozi hao ni: Dkt. Janeth Lekashingo, Mwenyekiti wa Tume ya Madini; Bi. Yokbeth Myumbilwa, Mwenyekiti wa Bodi ya GST; IGP Mstaafu Mheshimiwa Balozi Simon Sirro, Mwenyekiti wa Bodi ya STAMICO; Mheshimiwa Balozi Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya TEITI; Makamishna wa Tume ya Madini; na Wajumbe wa Bodi hizo.

**17. *Mheshimiwa Spika,*** nawapongeza Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini: Eng. Ramadhani Lwamo (Katibu Mtendaji, Tume ya Madini); Eng. Ally Samaje (Mtendaji Mkuu, GST); Dkt. Venance Mwasse (Mkurugenzi Mkuu, STAMICO); Bi. Mariam Mgaya (Katibu Mtendaji, TEITI); na Eng. Ally Maganga (Mratibu wa Kituo cha Jemolojia Tanzania) kwa kuzisimamia kwa makini na weledi taasisi wanazoziongoza. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Maafisa Madini Wakazi (RMO's) na Maafisa Migodi Wakazi (MRO's) kwa utekelezaji fanisi wa majukumu yao.

**18. *Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa naishukuru kwa moyo wa dhati familia yangu, mke wangu mpendwa Jacquelyne Moses Lupasa na watoto wangu Atarah na Allan kwa kunipa ushirikiano mkubwa na utulivu katika kusimamia majukumu yangu ya ubunge na uwaziri na kukubali kubeba baadhi ya majukumu ya familia.

**19. *Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa niungane na watanzania wenzangu kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama. Aidha, nitoe pole kwa Wananchi wa Dar es Salaam kwa kuondokewa na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Vilevile, nitoe pole kwa Wananchi wa jimbo la Isimani kwa kuondokewa

na aliyekuwa Mbunge wao na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi. Mwenyezi Mungu awarehemu marehemu na awape faraja familia na wananchi waliokuwa wakiongozwa nao.

***20. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watanzania wote kutokana na vifo, majeraha, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu kufuatia majanga mbalimbali yaliyosababishwa na mvua nyingi, ajali za barabarani, majini, moto na migodini.

***21. Mheshimiwa Spika***, napenda kuendelea kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini ambapo nchi yetu imeendelea kung'ara kimataifa na kuongeza imani kwa wawekezaji wa madini duniani. Kulingana na utafiti uliofanywa na Taasisi ya *Fraser* ya nchini Canada ambayo inaaminika kimataifa katika kutathmini mwenendo wa masoko ya uwekezaji wa madini, Tanzania ilishika nafasi ya 4 Afrika na ya 34 duniani katika kiashiria cha kuvutia uwekezaji (Investment Attractiveness Index - IAI) uliofanyika mwaka 2025. Aidha, kwa mujibu wa taarifa hiyo, Tanzania ilipata alama 68.04 mwaka 2025 ikilinganishwa na alama 62.75 katika mwaka 2024. Vilevile, kwa upande wa hazina za

rasilimali madini (mineral potential), Tanzania imeorodheshwa kuwa ya 15 duniani kwa kuwa na alama 75.

**22. *Mheshimiwa Spika,*** kulingana na Ripoti ya Uwekezaji Tanzania ya Mwaka 2025 (Tanzania Investment Report 2025), Sekta ya Madini imeendelea kuongoza katika thamani ya mtaji wa Uwekezaji Kutoka Nje (Foreign Direct Investment – FDI stock) katika mwaka 2024, ikiwa ni takriban robo tatu ya jumla ya mtaji wa uwekezaji katika sekta muhimu. Aidha, ripoti hiyo inaonesha kuwa kiwango cha mtaji kutoka nje katika Sekta ya Madini kiliongezeka hadi kufikia dola bilioni 9.79 mwaka 2024, kutoka dola bilioni 9.15 mwaka 2023 na dola bilioni 8.64 mwaka 2022. Ongezeko hilo limechangiwa na uhamasishaji na uwepo wa mazingira wezeshi kwa wawekezaji yaliyochochea upanuzi wa miradi iliyopo, uwekezaji wa faida inayopatikana na uunganishaji mitaji ndani ya sekta.

**23. *Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kupiga hatua muhimu ya kihistoria katika kuendeleza Madini Muhimu na Madini Mkakati ambapo Serikali imeingia makubaliano ya kutekeleza miradi ya madini mbalimbali ikiwemo *niobium*, nikeli, kinywe na dhahabu katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Mathalani, tarehe 24 Machi 2026, kwa mara ya kwanza Tanzania iliweza kushuhudia

kusainiwa kwa mkataba wa kuendeleza Madini Muhimu na Madini Mkakati kwa kusaini mkataba wa kuendeleza mradi wa uchimbaji wa madini ya *niobium* wa Panda Hill uliopo Mkoa wa Mbeya.

***24. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu utakuwa ni mradi mkubwa na wa kipekee katika bara la Afrika ambao utaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wanne (4) duniani. Mkataba huo ni kati ya Serikali na Kampuni ya Panda Hill Tanzania Limited. Uwekezaji wa awali katika mradi huo unakadiriwa kuwa dola za Marekani milioni 442 na unatarajiwa kuzalisha ajira zipatazo 1,600 na ajira 6,336 zisizo rasmi. Aidha, Serikali inatarajia kupata mapato ya takribani shilingi trilioni 2 kutokana na mrabaha, kodi na tozo, gawio la hisa za Serikali asilimia 16 zisizohafifishwa na kukuza matumizi ya bidhaa na huduma za ndani (local content) pamoja na uwajibikaji kwa jamii (CSR), ambapo thamani ya manunuzi ya ndani inatarajiwa kufikia dola za Marekani bilioni 1.77.

***25. Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi wa *niobium* utaiwezesha Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache duniani zinazochakata mbale na kuzalisha madini ya *niobium*. Aidha, madini hayo yana umuhimu mkubwa viwandani hususan katika kuongeza uimara wa chuma, matumizi ya teknolojia za kisasa ikiwemo vifaa vya elektroniki, magari ya umeme na injini za ndege.




**Picha Na. 2:** *Mheshimiwa Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini akisaini kwa niaba ya Serikali mkataba wa uchimbaji mkubwa wa madini ya Niobium utakaomilikiwa kwa ubia baina ya Serikali na Kampuni ya Panda Hill Tanzania Limited.*

***26. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Awamu ya Sita chini ya uongozi wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeshuhudia mageuzi makubwa na mafanikio ya hali ya juu katika Sekta ya Madini. Mchango wa sekta hii kwenye Pato la Taifa umeendelea kuimarika na kukua mwaka hadi mwaka ambapo mwaka 2023 mchango ulikuwa asilimia 9.1 na mwaka 2024 ulikuwa asilimia 10.1. Aidha, hadi kufikia kipindi cha robo tatu ya mwaka 2025 (Januari – Septemba) wastani wa mchango wa sekta umefikia asilimia 11.9.

***27. Mheshimiwa Spika,*** jitihada za kuimarisha usimamizi wa rasilimali zetu zimewezesha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kuongezeka kutoka shilingi 753,175,680,203.96 Mwaka wa Fedha 2023/2024 hadi kufikia shilingi 1,072,764,829,619.00 Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, hadi kufikia Machi 2026 shilingi 1,034,453,897,920.09 sawa na asilimia 114.94 ya lengo la makusanyo ya shilingi 900,000,000,000.00 kwa kipindi cha miezi tisa (9) zimekusanywa na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Mafanikio haya ni matokeo ya mikakati madhubuti ya Serikali ikiwemo kuimarisha usimamizi wa shughuli za Sekta ya Madini, kudhibiti utoroshwaji wa madini, kuhamasisha uwekezaji kwenye shughuli za madini na kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito.

***28. Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa masoko na vituo vya ununuzi wa madini kutoka masoko 43 na vituo 114 mwaka 2024/2025 hadi kufikia masoko 44 na vituo 118 mwaka 2025/2026. Kupitia masoko na vituo hivyo ilifanyika biashara ya madini yenye thamani ya shilingi 2,819,220,651,824.38 kwa mwaka 2024/2025 na shilingi 4,903,477,353,887.03 hadi kufikia Machi 2026.

***29. Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa salamu za shukrani, pongezi, pole na baadhi ya mafanikio ya Sekta

ya Madini, naomba sasa nijielekeze katika maeneo mahsusi ya hotuba hii ambayo ni: Mwenendo wa Biashara ya Madini Duniani; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## B. MWENENDO WA BIASHARA YA MADINI DUNIANI

**30. *Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa biashara ya madini duniani umeendelea kubadilika kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na mahitaji ya soko. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, bei ya madini ya dhahabu kwa wakia ilipanda hadi kufikia wastani wa dola za Marekani 4,190.47 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 2,655.80 katika kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kuongezeka kwa bei ya dhahabu kumetokana na sababu mbalimbali ikiwemo mahitaji makubwa ya madini hayo duniani kama njia ya kuhifadhi thamani ya fedha.

**31. *Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, bei ya madini ya almasi imeshuka na kufikia wastani wa dola za Marekani 159.84 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 168.95 kwa karati kwa kipindi kama hicho 2024/2025 sawa na upungufu wa asilimia 5.39. Mwenendo wa bei ya almasi

duniani umeendelea kukabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo: uwepo wa almasi ya viwandani (synthetic diamond) zilizosababisha kupungua kwa uhitaji wa almasi asilia hususani katika masoko makubwa duniani yakiwemo ya China na Marekani.

***32. Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa bei ya makaa ya mawe duniani umeendelea kukabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo kupungua kwa mahitaji ya makaa ya mawe katika soko la dunia. Hali hiyo imesababisha kushuka kwa bei ya makaa ya mawe kufikia wastani wa dola za Marekani 26.69 kwa tani ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 40.75 kwa tani kwa kipindi kama hicho 2024/2025 sawa na upungufu wa asilimia 34.50.

***33. Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa biashara ya madini ya Tanzanite duniani umeendelea kukabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo ukosefu wa masoko ya uhakika kutokana na vikwazo vya kibiashara duniani na uwepo wa vito vya kutengeneza viwandani. Hali hiyo imesababisha kushuka kwa bei ya madini ya Tanzanite kutoka wastani wa dola za Marekani 2,433.96 kwa kilogramu katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 na kufikia dola za Marekani 2,270.44 kwa kilogramu katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 sawa na upungufu wa asilimia 6.72.

***34. Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa madini mkakati na madini muhimu yakiwemo *lithium, cobalt, nickel, copper, aluminium, zinc, graphite,* na *rare earth elements* (REE), uhitaji umeendelea kuongezeka duniani ikilinganishwa na upatikanaji wake. Hali hii inasababishwa na ongezeko la matumizi katika teknolojia mbalimbali za kisasa na nishati safi ikiwemo uzalishaji wa magari ya umeme, betri za kuhifadhi nishati, vifaa vya kuzalisha umeme wa jua na wa upepo, pamoja na vifaa vya kiteknolojia kama vile simu janja, darubini na kompyuta.

***35. Mheshimiwa Spika,*** hali hii inatoa fursa kubwa kwa Tanzania kuhakikisha madini haya yanaongezwa thamani ndani ya nchi ili kuongeza mapato, ajira, na mchango wake katika uchumi wa Taifa. Serikali imeendelea kuchukua hatua za kimkakati ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje katika Sekta ya Madini.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### (i) Makadirio ya Mapato na Matumizi

***36. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bunge lako Tukufu liliidhinisha bajeti ya jumla ya shilingi 224,984,150,000.00 kwa Wizara ya Madini. Kati ya fedha hizo, shilingi 100,379,362,000.00 ni bajeti ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi 76,110,777,000.00

ni za matumizi mengineyo na shilingi 24,268,585,000.00 ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Aidha, shilingi 124,604,788,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi 71,507,708,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 53,097,080,000.00 ni fedha za nje.

***37. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,405,537,268,735.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,200,000,000,000.00 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi 205,537,268,735.00 zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**(ii) Fedha Zilizopokelewa na Kutumika**

***38. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imepokea jumla ya shilingi 82,902,605,920.35. Kati ya fedha hizo shilingi 10,476,255,954.31 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambazo ni fedha za ndani na shilingi 72,426,349,966.04 kwa ajili ya matumizi ya kawaida zikijumuisha shilingi 54,763,814,101.03 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 17,662,535,865.01 kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

***39. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara ilipokea na kutumia fedha za maendeleo shilingi 10,476,255,954.31 ikiwa ni fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali ambazo ni: ujenzi wa jengo la ofisi ya Afisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Geita; ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Tume ya Madini; ujenzi wa maabara ya kisasa ya uchunguzi wa miamba na madini ya GST katika eneo la Kizota, Dodoma; ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya Wizara na Tume ya Madini; ununuzi wa vifaa vya kupimia madini kwenye masoko ya madini; ununuzi wa vifaa mbalimbali vya jiosayansi kwa ajili ya GST; kufanya ulinganishi wa mapato ya Serikali na malipo ya kampuni za uziduaji ili kuandaa Ripoti ya TEITI ya Mwaka 2023/2024; na kumlipa Mshauri Elekezi aliyefanya Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira (SEA) kwenye Ikolojia ya Mikumi - Selous.

**(iii) Utekelezaji wa Vipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

***40. Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha Sekta ya Madini inaendelea kukua na kuwanufaisha watanzania ikiwa ni pamoja na kuendelea kuimarika kwa mchango wake kwenye Pato la Taifa, Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilijielekeza katika kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli; kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa;

kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini muhimu na madini mkakati; kuhamasisha uwekezaji na uongezaji thamani madini; kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito; kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za kina za madini; kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo; na kuzijengea uwezo Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini.

**(a) Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli**

***41. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilipangiwa kukusanya maduhuli ya shilingi 1,405,537,268,735.00 kutoka vyanzo mbalimbali. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,200,000,000,000.00 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina. Hadi kufikia Machi 2026 shilingi 1,034,453,897,920.09 sawa na asilimia 114.94 ya lengo la makusanyo ya shilingi 900,000,000,000.00 kwa kipindi cha miezi tisa (9) zimekusanywa na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 32 ikilinganishwa na shilingi 783,875,962,446.79 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, ili kuongeza maduhuli ya Serikali, Wizara imeimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, masoko ya madini, vituo vya ununuzi wa madini na mipaka ya nchi.

***42. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi zilizo chini ya Wizara zilipangiwa kukusanya na kutumia shilingi 205,537,268,735.00. Hadi kufikia Machi 2026 shilingi 61,850,652,766.87 zilikusanywa sawa na asilimia 40.12 ya lengo la makusanyo kwa kipindi rejewa. Lengo hilo halikufikiwa na STAMICO kutokana na kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa mikataba ya huduma ya uchorongaji; kushuka kwa bei ya makaa ya mawe kwenye soko la dunia; na Shirika kuchelewa kupokea mitambo ya kuzalisha nishati safi ya *Rafiki Briquettes* kutoka nje ya nchi. Aidha, kwa upande wa GST sababu zilikuwa ni kuharibika kwa vifaa vya maabara ikiwemo tanuru la kuchomea vyungu vya kuyeyushia sampuli za dhahabu (crucibles).

***43. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa kumekuwa na ongezeko la masoko na vituo vya ununuzi wa madini kutoka masoko 43 na vituo 114 Mwaka wa Fedha 2024/2025 hadi kufikia masoko 44 na vituo 118 Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kupitia masoko na vituo hivyo, ilifanyika biashara ya madini yenye thamani ya shilingi 4,903,477,353,887.03 hadi kufikia Machi 2026 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ikilinganishwa na shilingi 2,819,220,651,824.38 kwa kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

***44. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini nchini unaofanywa na baadhi ya wachimbaji na wafanyabiashara wa madini wasio waaminifu. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali imefanikiwa kukamata madini ya aina mbalimbali yenye thamani ya shilingi 3,314,024,775.00 katika matukio 55 kwenye Mikoa ya kimadini ya Kahama, Mwanza, Geita, Dar es Salaam, Arusha, Songwe, Mbeya, Iringa, Mirerani, Mahenge, Chunya, Kagera, Manyara, Mbogwe na Morogoro. Aidha, madini yaliyokamatwa yalitaifishwa na Serikali na watuhumiwa walifikishwa kwenye vyombo vya Sheria.

***"Ni rai yangu kwa wachimbaji na wafanyabiashara wa madini kuzingatia Sheria za Nchi kuhusiana na biashara ya madini"***

***45. Mheshimiwa Spika,*** mapato ya fedha za kigeni yatokanayo na mauzo ya madini nje ya nchi yamekuwa yakiimarika mwaka hadi mwaka. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 5,401.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 4,119.9 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 31.1. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu na madini mengine. Aidha, mwaka 2025 thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi yalichangia asilimia 52.57 ya mauzo yote ya bidhaa za asili na zisizo za asili yaliyouzwa nje

ikilinganishwa na asilimia 45.17 mwaka 2024. Vilevile, kwa upande wa mauzo ya bidhaa zisizo za asili pekee, Sekta ya Madini ilichangia asilimia 63.73 mwaka 2025 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 56.99 mwaka 2024. Pia, thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 3,419.6 mwaka 2024 na kufikia dola za Marekani milioni 4,753.9 mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia 39.0.

***46. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya vibali 8,635 vya usafirishaji madini nje ya nchi vilitolewa. Madini yaliyosafirishwa ni pamoja na dhahabu, almasi, vito ghafi, vito vilivyokatwa na kusanifiwa, madini ya viwandani, madini ya bati, madini ya shaba na makaa ya mawe yenye jumla ya thamani ya shilingi 9,918,801,252,974.08. Aidha, katika kipindi rejewa, jumla ya vibali 195 vya kuingiza madini nchini vyenye thamani ya dola za Marekani 23,299,887.92 vilitolewa. Madini yaliyopata vibali vya kuingizwa nchini kwa kiwango kikubwa ni pamoja na *copper cathodes*, *loaded carbons* na *ferro-silicon manganese*.

**(b) Kuongeza Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa**

***47.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa umekuwa ukiimarika mwaka hadi mwaka. Mchango huo uliongezeka kutoka asilimia 9.1 mwaka 2023 na kufikia asilimia 10.1 mwaka 2024. Aidha, hadi kufikia kipindi cha robo tatu ya mwaka 2025 (Januari – Septemba) wastani wa mchango wa sekta umefikia asilimia 11.9. Mwenendo huu umechangiwa ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa usimamizi wa Sekta ya Madini, na kuongezeka kwa uwekezaji na uzalishaji.

**(c) Kuendeleza Mnyororo wa Thamani katika Madini Muhimu na Madini Mkakati**

***48.*** ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada mbalimbali zimeendelea kufanyika kuhakikisha Madini Muhimu na Madini Mkakati yananufaisha Taifa. Jitihada hizo ni pamoja na kufanya tafiti; kutangaza fursa za uwekezaji; na kutoa leseni za utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na biashara ya madini muhimu na madini mkakati zilizopo nchini. Aidha, Wizara inaendelea na taratibu za kuidhinishwa orodha ya Madini Muhimu na Madini Mkakati Tanzania ili iweze kutumika katika usimamizi wa rasilimali za madini hayo.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni 454 za Madini Muhimu na Madini Mkakati yakiwemo madini ya kinywe (271), *nickel* (136), *cobalt* (2), *lithium* (6), *heavy mineral sands* (11) na *rare earth elements* (28). Utoaji wa leseni hizi unaendelea kuweka msingi thabiti wa kukuza uwekezaji katika utafutaji na uendelezaji wa madini muhimu na madini mkakati nchini, sambamba na kuimarisha jitihada za Serikali za kukuza uchimbaji endelevu, kukuza uongezaji thamani wa madini, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali pamoja na mchango wa Sekta ya Madini katika maendeleo ya uchumi wa Taifa.

**(d) Kuhamasisha Uwekezaji na Uongezaji Thamani Madini**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha uwekezaji nchini, Wizara ilitangaza fursa za uwekezaji na kutoa elimu kwa Umma kupitia ziara mbalimbali za viongozi, vyombo vya habari na kwenye mikutano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Wizara ilishiriki kwenye mikutano, makongamano na maonesho ya kimataifa nane (8) ambayo ni: Mkutano wa *Future Minerals Forum* – Saudi Arabia; *Mining Indaba* – Afrika Kusini; Mkutano wa 13 wa Kimataifa wa Madini na Nishati - Zambia (Zambia International Mining and Energy Conference – ZIMEC); *Prospectors and Developers Association of Canada*

(PDAC) – Canada; kushiriki mikutano ya Umoja wa Nchi za Afrika zinazozalisha Almasi (ADPA); *Africa Down Under* – Australia; *The International Conference on the Great Lakes Region* (ICGLR) – DRC na Uganda; na kwenye Maonesho ya 69 ya Vito na Usonara yaliyofanyika jijini Bangkok nchini Thailand.




**Picha Na. 3:** *Mheshimiwa Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini (katikati) katika picha ya pamoja na wawakilishi wa kampuni ya kimataifa ya uchimbaji madini ya dhahabu ya barrick baada ya Mkutano wa Kimataifa wa "African Mining Indaba". Upande wa kulia ni Bw. Msafiri Mbibo. Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Madini, wa pili kulia ni Mheshimiwa CPA. Simon Songe (Mb.), Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na upande wa kushoto ni Dkt. Venance Mwasse, Mkurugenzi Mtendaji STAMICO.*

**51. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliandaa na kushiriki mikutano na maonesho ya ndani matano (5) ambayo ni: Maonesho ya 32 ya NaneNane Mkoani Dodoma; Maonesho ya nane (8) ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini yaliyofanyika mjini Geita; Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Sabasaba yaliyofanyika Dar es Salaam; Maonesho ya "*SAMIA CONNECT*" Jijini Arusha; na maonesho ya Kimataifa ya Biashara Zanzibar. Washiriki waliotembelea mabanda ya Wizara na taasisi zake walipata elimu kuhusu majukumu, sera, sheria na miongozo mbalimbali inayosimamia Sekta ya Madini pamoja na kufahamu fursa za uwekezaji zilizopo.

**52. Mheshimiwa Spika,** kupitia mikutano hiyo kampuni mbalimbali zilionesha nia ya kuwekeza nchini na washiriki walipata nafasi ya kujifunza na kuongeza ujuzi kuhusu matumizi ya teknolojia za kisasa katika shughuli za madini, kujenga na kukuza diplomasia ya uchumi ambayo ni msingi wa ustawi wa biashara na uwekezaji baina ya nchi yetu na nchi nyingine.

**53. Mheshimiwa Spika,** watanzania na wadau wameendelea kuelimishwa na kufahamishwa kuhusu uwepo wa fursa za uwekezaji katika Sekta ya Madini nchini ikiwemo sheria, kanuni na miongozo inayosimamia sekta. Aidha, elimu imeendelea kutolewa kupitia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwa ni pamoja na Jarida la Mtandaoni la

Madini na Uchumi, programu maalumu za urushwaji wa vipindi mubashara vilivyoelezea masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Madini. Vyombo hivyo ni pamoja na *TBC, Clouds Media, Crown Media, ITV, Kiss FM, Azam Media, Wasafi Media, VOA, BBC, DW, TRT, Radio France, ZBC* na *Morning Star.*

**54. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha juhudi za kuelimisha umma na wadau kuhusu maendeleo ya Sekta ya Madini pamoja na fursa zilizopo katika uwekezaji na ushiriki wa wananchi. Ili kufikia azma hiyo, Wizara imeanzisha na kuendesha majukwaa maalum ya mawasiliano ya kidijitali yanayolenga kutoa elimu na taarifa sahihi kwa jamii. Miongoni mwa majukwaa hayo ni mfululizo wa makala za video (Documentary) zinazojulikana kama "*Madini Diary*", zinazoangazia kwa kina shughuli mbalimbali za Sekta ya Madini, ubunifu wa teknolojia, mafanikio ya wadau na mchango wa sekta katika maendeleo ya Taifa.

**55. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeanzisha *podcast* ya "Madini Safari" ambayo hutumika kama jukwaa la majadiliano na wataalam, wachimbaji, wawekezaji na wadau wengine ili kutoa uelewa wa kina kuhusu maendeleo ya Sekta ya Madini nchini. Kupitia majukwaa hayo, Wizara imeendelea kuongeza uelewa kwa umma, kuhamasisha uwekezaji na kuimarisha ushiriki wa

wananchi katika kunufaika na rasilimali madini kwa maendeleo ya Taifa.

***56. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini zinaimarika na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa, Wizara ilifanya yafuatayo: kuendelea kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini ya vito ambapo madini ghafi yenye uzito wa zaidi ya gramu mbili (2) yanatakiwa yaongezewe thamani ndani ya nchi kabla ya kusafirishwa nje ya nchi; kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha matumizi ya madini ya viwandani yanayotumika katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ambapo kwa sasa uzalishaji wa madini ya chokaa, jasi, udongo mwekundu unaotumika kutengeneza *clinker* kwa ajili ya kuzalisha saruji umeongezeka; kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezaji wa bidhaa za madini; na kuendelea kutoa ushirikiano kwa wamiliki wa viwanda vya usafishaji wa madini ya dhahabu nchini ili kupata ithibati ya LBMA.

***57. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha uandaaji wa Mkakati wa Uongezaji Thamani Madini. Mkakati huo unatoa mwelekeo kwa Serikali wa kubadilisha Sekta ya Madini kutoka kwenye uuzaji wa madini ghafi na kuelekea kwenye kuuza madini yaliyoongezewa thamani ndani ya nchi. Lengo kuu ni kutumia rasilimali madini kama njia ya

kufungamanisha Sekta ya Madini na Sekta nyingine za kiuchumi ikiwemo viwanda. Utekelezaji wa mkakati huo utachochea ongezeko la thamani ya madini yetu na kuongeza viwanda vitakavyosaidia upatikanaji wa ajira, Pato la Taifa, ubunifu, kuongeza ujuzi na kuimarisha ushindani wa bidhaa zitokanazo na madini katika masoko ya ndani na nje ya nchi kupitia mnyororo imara wa uongezaji thamani.

***58. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia shughuli za uongezaji thamani madini nchini kupitia viwanda sita (6) vya kusafisha dhahabu (refinery) vilivyopo mikoa ya Dodoma (1), Shinyanga (1), Geita (2), Dar es Salaam (1) na Mwanza (1). Aidha, Wizara inaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuyeyusha madini ya Shaba, Nikeli, Bati na Chumvi katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Kagera, Mbeya, Lindi na Pwani. Sambamba na hilo, Wizara inaendelea kushirikiana na wamiliki wa viwanda vya kusafisha dhahabu ili kupata ithibati ya LBMA kwa ajili ya kuwezesha viwanda hivyo kutambulika katika masoko ya kimataifa.

***59. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha shughuli za uongezaji thamani madini ya vito na metali za thamani nchini kwa kuendelea na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa jengo pacha la ghorofa 8 katika Kituo cha Jemolojia Tanzania ili kuongeza

uwezo wa kutoa mafunzo. Ujenzi huo upo katika hatua ya ukamilishaji wa msingi (basement). Aidha, Wizara kupitia TGC inaendelea na taratibu za ununuzi wa viwanja viwili (2) kwa ajili ya upanuzi wa eneo la Kituo vyenye ukubwa wa mita za mraba 7,318 ambavyo vipo mkabala na eneo la ujenzi.

### (e) Kuimarisha Uendeshaji wa Minada na Maonesho ya Madini ya Vito

**60. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) iliendesha mnada mmoja (1) wa ndani wa madini ya vito uliofanyika kielektroniki Jijini Arusha Mwezi Novemba 2025. Katika mnada huo madini yenye thamani ya shilingi 231,250,000.00 yalinunuliwa. Wizara inaendelea kuhamasisha na kuongeza mwamko wa ushiriki wa wadau katika minada ya madini ya vito. Aidha, Wizara imeunda timu ndogo ya uhamasishaji na ufuatiliaji wa uzalishaji wa madini ya vito ikijumuisha maandalizi ya Mnada wa Kimataifa na Maonesho ya Madini ya Vito ya Arusha (Arusha Gem Fair) unaotarajiwa kufanyika mwezi Juni 2026.

**(f) Kuongeza Uwekezaji kwenye Tafiti za Kina za Madini**

***61. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia GST imefanya utafiti wa jiofizikia kwa kutumia ndege nyuki katika maeneo ya Geita, Manyara na Lindi ambapo taarifa muhimu za kina za jiolojia zilibainishwa katika maeneo hayo. Sambamba na hilo, umefanyika pia utafiti wa kina wa jiofizikia (High Resolution Airborne Geophysical Survey) katika maeneo ya leseni za STAMICO zilizoko Mkoa wa Lindi, hatua inayolenga kuongeza uelewa wa kina kuhusu rasilimali zilizopo. Utafiti huo uliofanyika umewezesha Serikali kubaini uwezekano wa matumizi ya ndege nyuki kutumika katika upatikanaji wa taarifa za kina za jiofizikia kwenye leseni ndogo za uchimbaji wa madini. Hivyo, hatua hii itasaidia kutumia teknolojia ya ndege nyuki katika kupata taarifa za kina za jiofizikia kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo.

***62. Mheshimiwa Spika,*** GST imekamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia katika vitalu viwili (2) vya kimkakati vilivyoko kusini-magharibi mwa nchi, vyenye ukubwa wa takribani kilomita za mraba 176,676.45 sawa na asilimia 18 ya eneo lote la nchi. Utekelezaji wa utafiti huu unatarajiwa kuongeza upatikanaji wa taarifa za kina za jiofizikia kutoka asilimia 16 ya sasa hadi kufikia asilimia 34.

***63. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kutokuwepo kwa taarifa za kina za jiofizikia kwenye baadhi ya maeneo ya nchi, Wizara imeendelea kuhamasisha kampuni mbalimbali kufanya tafiti za kina kwenye maeneo ya leseni zao kama hatua za awali za utafutaji madini. Mathalani, hivi karibuni kampuni ya Barrick imefanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa kutumia helikopta katika maeneo ya Msalala, Nzega, Igunga, Mbogwe na Nyang'hwale kwa ajili ya kubaini uwepo wa maeneo mapya yenye madini. Utafiti huo umelenga kubaini uwezekano wa maeneo mapya ya miradi ya uchimbaji wa dhahabu.




**Picha Na. 4:** *Mheshimiwa Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini akizindua mradi wa utafiti wa kina wa madini kwa kurusha helikopta unaotekelezwa na Kampuni ya Barrick.*

***64. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia GST imeendelea na ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi na Usambazaji wa Taarifa za Jiosayansi na Rasilimali za Madini ambapo hadi kufikia Machi 2026 ujenzi wa mfumo huo umefikia asilimia 45. Aidha, kukamilika kwa mfumo huo kutaimarisha usimamizi na upatikanaji wa taarifa za miamba na madini iliyopo nchini.

**(g) Kuwarasimisha na Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo**

***65. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya leseni 8,878 za uchimbaji mdogo zimetolewa na Wizara kupitia Tume ya Madini. Aidha, STAMICO inaendelea kusaidia wachimbaji wadogo kwa kutoa huduma za kitaalam katika utafiti, uchimbaji, uchenjuaji na utunzaji wa mazingira. Katika kipindi husika jumla ya wachimbaji 451 wamepatiwa mafunzo kupitia vituo vya mfano vya Lwamgasa, Katente na Itumbi.

***66. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia STAMICO imetoa huduma ya uchorongaji katika maeneo mbalimbali, ambapo jumla ya mita 3,896.59 zilichorongwa. Kwa upande wa wazalishaji chumvi wadogo, ujenzi wa kiwanda cha kusafisha chumvi kilichopo Nangurukuru Wilaya ya Kilwa umekamilika, na hatua inayofuata ni kukamilisha usimikaji wa mitambo.

***67. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Madini imefanya ufuatiliaji wa kutambua maeneo ya kugawiwa kwa wachimbaji wadogo ambapo hadi sasa jumla ya maeneo 99 yamependekezwa kwa ajili ya uchambuzi. Aidha, maeneo mawili (2) yametengwa katika Mikoa ya kimadini ya Mbogwe - Msasa (Leseni 35 zimetolewa) na Lindi - Ntaka Hill (Leseni 69 zimetolewa).

***68. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya wazalishaji chumvi 576 kutoka Mkoa wa Lindi na Mtwara, na wachimbaji wadogo 976 kutoka Mbogwe na Geita Mjini wamepewa mafunzo kuhusu utafiti, uchimbaji salama, uchenjuaji, afya, usalama na utunzaji wa mazingira migodini.

***69. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kuwezesha ushiriki wa wachimbaji wadogo katika warsha, makongamano, mikutano na majukwaa ya kitaifa na kimataifa kwa ajili ya kujifunza teknolojia mbalimbali pamoja na kutafuta fursa za biashara. Mathalani, chini ya uratibu wa FEMATA, jumla ya wachimbaji wadogo 31 walifanya ziara ya mafunzo nchini Uturuki kuanzia tarehe 3 hadi 14 Septemba 2025.

***70. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kupitia Tume ya Madini imesaini Hati ya Makubaliano na Benki ya CRDB kwa ajili ya upatikanaji wa mikopo kwa wachimbaji wadogo wa madini.

Kama sehemu ya utekelezaji wa makubaliano hayo kikundi cha wachimbaji wadogo cha *Songwe Gold Family* – Saza mkoani Songwe kinatarajiwa kupata mkopo wa shilingi bilioni 50 kutoka benki ya CRDB.

***"Nitumie fursa hii kuzishukuru benki za CRDB, NMB, NBC, AZANIA na KCB kwa kuendelea kuwakopesha wachimbaji wadogo. Aidha, naomba kutoa wito kwa benki nyingine nchini kuendelea kuwaamini na kuwakopesha wachimbaji wadogo"***




**Picha Na. 5:** *Mheshimiwa Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini akishuhudia utiaji saini wa makubaliano maalum ya kuwakopesha wachimbaji wadogo kati ya Tume ya Madini na Benki ya CRDB.*

### (h) Kuzijengea Uwezo Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ya Madini

**71. *Mheshimiwa Spika,*** Rasilimaliwatu ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha utendaji kazi unaimarika na malengo ya Wizara yanafikiwa. Hivyo, Wizara pamoja na Taasisi zake imeendelea kusimamia utendaji kazi na maslahi ya watumishi wake pamoja na kujaza nafasi zilizo wazi. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara na Taasisi zake imejaza nafasi 147 kwa utaratibu wa uhamisho (55) na ajira mpya (92). Aidha, kupitia uhamisho huo, Wizara imepata watumishi (24), Tume ya Madini (17), TEITI (8) na GST (6). Vilevile, kwa upande wa Ajira mpya Wizara imepata watumishi (9), STAMICO (1), Tume ya Madini (66), GST (12) na TGC (4). Pia, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zilizo chini yake imeendelea kusimamia na kuhakikisha maslahi na stahiki za watumishi zinapatikana kwa wakati.

**72. *Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mafunzo kwa watumishi, Wizara na Taasisi zake zimewawezesha watumishi 455 kupata mafunzo. Kati ya hao watumishi 347 walipata mafunzo ya muda mfupi na 108 ya muda mrefu katika masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Madini.

***73. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa Taasisi zilizo chini yake zinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuzipatia vitendea kazi. Tume ya Madini imewezeshwa vifaa vya masoko na TEHAMA; STAMICO imewezeshwa kupata leseni mbili za utafiti wa madini ya nikeli na adimu (REE); GST imewezeshwa upatikanaji wa vitendea kazi kwa ajili ya utafiti wa madini ikiwemo magari manne (4); TGC imewezeshwa kuboresha miundombinu ya kutolea mafunzo, huduma za uzalishaji wa bidhaa kwa lengo la kukuza shughuli za uongezaji thamani madini nchini; na TEITI imewezeshwa kwa kupewa jengo kwa ajili ya ofisi lililopo mji wa Serikali Mtumba.



**Picha Na. 6**: *Magari mapya manne (4) kwa ajili ya kuimarisha shughuli za utafiti GST.*

***74. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na taratibu za kuidhinishwa kwa TGC kuwa Taasisi inayojitegemea. Hatua hii itaiwezesha TGC kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

## (iv) Utekelezaji wa Maeneo Mengine ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2025/2026

***75. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imetekeleza majukumu yake mengine kama ifuatavyo:

### (i) *Mining Vision* 2030: Madini ni Maisha na Utajiri

***76. Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia matarajio ya DIRA 2050, Wizara imekamilisha Andiko la *Mining Vision 2030* lililozingatia nguzo tano (5) ambazo ni: kuwa na taarifa za jiosayansi; kuimarisha mfumo wa kisheria na kitaasisi; kuimarisha ufungamanishaji wa Sekta ya Madini na sekta nyingine za kiuchumi na uwekezaji; kukuza uchimbaji mdogo wa madini; na kuimarisha usimamizi wa mazingira.

### (ii) Programu ya *Mining for a Brighter Tomorrow* – MBT

***77. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanza kutekeleza Mpango wa MBT ambao ni wa miaka mitano kuanzia mwaka 2025/2026 hadi 2029/2030. Mpango huo unalenga kuongeza ushiriki wa vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalum katika mnyororo wa thamani kwenye Sekta ya Madini. Aidha, Malengo Mahsusi ya Mpango wa MBT ni pamoja na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya sekta, kujenga uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za mnyororo wa thamani wa madini, na kuimarisha ujumuishi na manufaa yatokanayo na Sekta ya Madini kwa vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalum.

***78. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza malengo ya Mpango wa MBT, Wizara imetoa jumla ya leseni 273 za uchimbaji wa madini kwa vikundi 183 vyenye jumla ya wanavikundi 2,550 katika mikoa mbalimbali ikiwemo Mara, Kagera, Shinyanga, Morogoro, Dodoma na Njombe. Aidha, Wizara ilitoa elimu kuhusu usalama, afya, utunzaji wa mazingira na usimamizi wa rasilimali fedha kwa wanufaika wa leseni zilizotolewa. Vilevile, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa makundi hayo kupitia miradi mbalimbali ya uchimbaji na biashara ya madini ikiwemo mradi wa Nyamongo kwa kushirikiana na Mgodi wa dhahabu wa

*North Mara* katika Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara. Sambamba na hilo, mpango huu unatekelezwa katika maeneo ya Mirerani Mkoa wa Manyara, Mbogwe na Nyang'hwale Mkoa wa Geita. Wizara pia imeendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa MBT.

**(iii) Kuwajengea Uwezo Wataalam kwenye Maeneo Muhimu katika Sekta ya Madini**

***79. Mheshimiwa Spika,*** ili kukidhi mahitaji ya wataalam na uwepo wa teknolojia mahsusi katika mnyororo wa thamani wa madini nchini, Wizara imekamilisha taratibu za kuwapeleka wataalamu masomoni ndani na nje ya nchi katika fani mbalimbali zikiwemo: ukadiriaji wa mashapo (resource estimation); modeli za kifedha (financial modelling); ukaguzi na usimamizi wa rasilimali madini; uthaminishaji wa madini; ukataji wa madini ya vito; utengenezaji wa bidhaa za usonara na uongezaji thamani madini. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara imepanga kuwajengea uwezo jumla ya watumishi nane (8) katika maeneo ya ukadiriaji mashapo (resource estimation), modeli za kifedha (financial modelling) na ukaguzi wa fedha (financial auditing) migodini.

### (iv) Kuboresha Usimamizi wa Shughuli za Madini Kidijitali

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea na taratibu za kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Sekta ya Madini Kidijitali utakaojulikana kama "*Mineral Sector Management Information System* - MSMIS". Mfumo huu unalenga kuimarisha usimamizi, uratibu na upatikanaji wa taarifa za Sekta ya Madini kwa kutumia teknolojia za kidijitali, sambamba na jitihada za Serikali za kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za umma. Hatua za awali zimeanza kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kufanya uchambuzi wa mahitaji ya mfumo, kubainisha wadau watakaohusika katika utekelezaji wa mfumo na maandalizi ya nyaraka muhimu zinazohitajika.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mfumo huo, Wizara pamoja na Taasisi zake inatarajia kupata manufaa mbalimbali ikiwemo kuwepo kwa jukwaa la pamoja la kidijitali litakalorahisisha ukusanyaji, uchakataji, uhifadhi na usambazaji wa taarifa za Sekta ya Madini kwa ufanisi na kwa wakati. Aidha, mfumo utasaidia kuweka usimamizi thabiti wa taarifa zinazohusiana na utoaji wa leseni za uchimbaji madini, uzalishaji wa madini, biashara na masoko ya madini, na mapato yatokanayo na shughuli za madini. Vilevile, mfumo huo utaongeza uwazi na uwajibikaji

katika usimamizi wa rasilimali za madini kwa kuwezesha ufuatiliaji wa karibu wa shughuli za wadau wa Sekta ya Madini.

***82. Mheshimiwa Spika,*** manufaa mengine yatakayopatikana kutokana na uanzishwaji wa Mfumo wa MSMIS ni pamoja na kuiwezesha Serikali kufanya maamuzi sahihi ya kisera na kiutendaji kwa kuzingatia takwimu na taarifa sahihi zinazopatikana kwa wakati. Sambamba na hayo mfumo husika utapunguza utegemezi wa mifumo ya kianalojia, kurahisisha upatikanaji wa taarifa na kuboresha uratibu kati ya taasisi mbalimbali za Serikali zinazohusika na usimamizi wa Sekta ya Madini. Mfumo huo utaunganishwa na mifumo mingine ya Serikali ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa shughuli za madini na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**(v) Mpango Mkakati wa Madini Muhimu na Madini Mkakati (Critical and Strategic Minerals Strategy)**

***83. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imekamilisha Mpango Mkakati wa Madini Muhimu na Madini Mkakati. Utekelezaji wake utaanza kutumika mara baada ya kuidhinishwa kwa orodha ya Madini Muhimu na Madini Mkakati. Mkakati huo ni moja ya nyenzo za kutekeleza Sera ya Madini iliyohuishwa

pamoja na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Muda Mrefu (LTPP 2050) ili kufikia malengo ya DIRA 2050.

### (vi) Marekebisho ya Sheria ya Madini Sura 123 na Kanuni zake

***84. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, Wizara imefanya marekebisho ya Kanuni za Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii za Mwaka 2025 na kutangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 692 la tarehe 19 Desemba, 2025. Baadhi ya marekebisho yaliyofanyika ni pamoja na kurekebisha kanuni ya 6 ili kuboresha muundo wa kamati ya wataalamu kwa lengo la kuongeza ufanisi.

***85. Mheshimiwa Spika,*** marekebisho mengine ni kuongeza kanuni ndogo ya 7(3) iliyolenga kupunguza gharama za utendaji wa kamati ya wataalamu na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa miradi kwa kuelekeza kila taasisi imgharamie mwakilishi wake. Kanuni za 8 na 9 zimeboreshwa kwa kuweka ukomo wa muda wa kuwasilisha mipango, kanuni ya 15 imefutwa na kutungwa kanuni mpya inayofafanua vizuri zaidi majukumu ya wamiliki wa leseni za madini ikiwemo kuwasilisha taarifa za fedha na miradi. Pia, kanuni ndogo ya 16(6) inayohusu usimamizi, ufuatiliaji na ukaguzi wa utekelezaji wa mipango ya wajibu wa wenye leseni kwa jamii imeongezwa.

**86. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetunga Kanuni kuhusu marekebisho ya Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania katika shughuli za madini za mwaka 2025 na kutangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 563 la tarehe 12 Septemba, 2025. Lengo la marekebisho hayo ni kuimarisha na kuongeza ushiriki wa watanzania katika shughuli zote za mnyororo wa thamani wa Sekta ya Madini na kuongeza mamlaka ya Tume ya Madini ya kuidhinisha, kusimamia na kufuatilia mipango ya ubia kati ya watanzania na kampuni za kigeni ili kuhakikisha kuwa watanzania wanafaidika na mipango hiyo ya ubia. Pia, marekebisho hayo yanaipa mamlaka Tume ya Madini kutangaza kwa kadri itakavyoonekana inafaa bidhaa na huduma ambazo zinatakiwa kutolewa na watanzania au kampuni zinazomilikiwa na watanzania kwa asilimia 100.

**87. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, Wizara imetunga kanuni mpya, Kanuni za Leseni Ndogo ya Uchenjuaji wa Madini za Mwaka 2025 na kutangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 572 la tarehe 12/9/2025. Kanuni hizi zinazosimamia leseni ndogo za uchenjuaji wa madini zitaboresha shughuli za Sekta ya Madini kwa kuwatambua na kutoa leseni kwa wachenjuaji wadogo. Kanuni hizi zinazuia uchenjuaji holela uliokuwa unafanywa bila kuzingatia miongozo na taratibu za kiafya, usalama na utunzaji mazingira.

### (v) Utekelezaji wa Shughuli za Taasisi Zilizo Chini ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**88. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuzisimamia na kuziwezesha taasisi zake tano (5) ili ziendelee kutekeleza majukumu kwa ufanisi na kuzingatia Sera, Sheria na Miongozo inayosimamia Sekta ya Madini. Taasisi hizo ni Tume ya Madini; Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST); Shirika la Madini la Taifa (STAMICO); Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC); na Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI). Taarifa ya utekelezaji wa taasisi ni kama ifuatavyo:

#### a. TUME YA MADINI

**89. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 Tume ya Madini imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

##### (i) Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini

**90. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Tume ya Madini ilitoa jumla ya leseni 11,674 ikilinganishwa na lengo la kutoa leseni 11,463. Leseni zilizotolewa ni kama ifuatavyo: Leseni za Uchimbaji wa Kati wa Madini (MLs) - 21; Leseni za Utafutaji wa Madini (PLs) - 313; Leseni za Uchimbaji Mdogo (PMLs) – 8,878; Leseni za Uchenjuaji wa Madini (PCLs) - 41; Leseni

za Biashara Kubwa ya Madini (Dealer License - DLs) - 914 na Leseni za Biashara Ndogo ya Madini (Broker License - BLs) – 1,507.

***91. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, leseni 111 za utafutaji wa madini na leseni 35 za uchimbaji wa kati wa madini zilipewa hati za makosa kutokana na kutozingatia masharti ya leseni ikiwa ni pamoja na kutolipa ada za mwaka na kutoendeleza maeneo ya leseni. Aidha, leseni 53 za utafutaji madini na leseni 29 za uchimbaji wa kati wa madini zilifutwa baada ya wamiliki wake kushindwa kurekebisha makosa yao.

**(ii) Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Madini katika Uzalishaji na Biashara ya Madini**

***92. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 madini yenye thamani ya shilingi 16,245,437,499,141.10 yalizalishwa na kuuzwa. Kutokana na thamani hiyo, Serikali iliweza kukusanya jumla ya shilingi 957,396,031,069.62. Kati ya fedha hizo shilingi 835,190;241,847.76 ni malipo ya mrabaha na shilingi 122,205,789,221.86 ni malipo ya ada ya ukaguzi. Uwiano wa uzalishaji kwa baadhi ya madini ni kama ifuatavyo: Dhahabu uzito wa kilo 51,819 yenye thamani ya shilingi 13,519,000,571,509.00; makaa ya mawe tani 2,201,441 yenye thamani ya shilingi 699,950,878,624.00; madini

ujenzi tani 30,215,970 yenye thamani ya shilingi 535,707,335,599.00; madini ya viwandani tani 12,269,218 yenye thamani ya shilingi 364,041,807,755.00; almasi karati 294,865 yenye thamani ya shilingi 109,315,499,461.00; na madini mengine mbalimbali yenye thamani ya shilingi 1,017,421,406,193.10.

***93. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi rejewa, Tume ya Madini kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za Serikali iliendelea kusimamia utendaji kazi wa masoko ya madini 44 na vituo vya ununuzi wa madini 118 ili kuhakikisha yanafanya kazi kwa ufanisi. Kupitia masoko na vituo vya ununuzi wa madini, Tume ya Madini ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 292,482,721,083.67 ikijumuisha shillingi 259,634,483,324.52 ikiwa ni mrabaha na shilingi 32,848,237,759.15 ada ya ukaguzi kutokana na mauzo ya madini yenye thamani ya shilingi 4,903,477,353,887.03.

### (iii) Ukaguzi wa Masuala ya Usalama, Afya na Mazingira

***94. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, ukaguzi wa migodi kuhusu usalama, afya, mazingira na matumizi salama ya baruti ulifanyika. Ukaguzi huu ulihusisha migodi mikubwa sita (6), migodi ya kati 31 na migodi midogo 9,080 katika maeneo mbalimbali kwenye mikoa 30 ya kimadini nchini.

***95. Mheshimiwa Spika,*** katika kaguzi hizo masuala mbalimbali yalibainika ikiwa ni pamoja na: kukosekana kwa mpango wa ufungaji mgodi uliohuishwa; kutotekelezwa kikamilifu kwa matakwa ya Sheria ya Baruti; kukosekana kwa taarifa za usanifu wa maeneo ya kuhifadhi miambataka pamoja na mabwawa ya topetaka; kukosekana kwa meneja mgodi aliyeteuliwa kwa mujibu wa utaratibu; maduara kutokuwa na miundombinu ya kiusalama; na vifaa kinga kutotumiwa ipasavyo. Wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu yaliyobainika ili kukidhi matakwa ya Sheria ya Madini Sura 123, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 pamoja na Sheria ya Baruti Sura 45.



**Picha Na. 7:** *Maafisa wakikagua masuala ya Usalama, Afya na Mazingira katika mgodi wa chini ya ardhi wa Polygold Co. LTD uliopo Musoma, Mara.*

***96. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, ukaguzi ulifanyika katika maghala ya kuhifadhia baruti kwenye mikoa ya kimadini ya Kahama, Geita, Katavi, Kigoma, Manyara, Mirerani, Simiyu, Tanga, Mwanza, Mara, Tabora na Mbeya. Jumla ya maghala ya kuhifadhia baruti 678, bohari 145, Stoo 295 na masanduku 280 yalikaguliwa. Katika kaguzi hizo masuala mbalimbali yalibainika ikiwemo kukosekana kwa vipima joto ndani ya maghala, vinasa radi pamoja na uhifadhi wa baruti kuzidi

uwezo wa maghala na wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo.

***97. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya vibali 428 vya baruti vilitolewa. Kati ya vibali hivyo, vitano (5) ni vya kuuza baruti, 311 vya kuingiza baruti nchini, 81 vya kutoa baruti nchini kwenda nje ya nchi na 31 vya kusafirisha baruti kupitia nchini kwenda nchi nyingine. Vibali husika vilitolewa baada ya maombi kukidhi matakwa ya Sheria ya Baruti, Sura 45.

***98. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, maombi ya vibali 27 vya ujenzi wa hifadhi za baruti, kutengeneza, kuuza, kutunza na kutumia baruti yalipokelewa na kufanyiwa kazi katika mikoa ya kimadini 13. Kati ya maombi hayo, 21 yalikidhi vigezo na sita (6) hayakukidhi vigezo na wahusika walielekezwa kufanya marekebisho.

***99. Mheshimiwa Spika,*** maeneo manne (4) ya kuhifadhia miambataka yalikaguliwa kwa lengo la kuhakiki ubora na kutoa idhini ya matumizi katika Mikoa ya Geita, Kahama, Singida na Dodoma. Vilevile, mabwawa ya topetaka (TSF) 31 yalikaguliwa kwa lengo la kutoa idhini ya ujenzi au matumizi. Ukaguzi huo ulilenga kuangalia na kujiridhisha maeneo yaliyopendekezwa iwapo yanafaa kwa ajili ya ujenzi pamoja na kuangalia hatua za ujenzi kama

zimekidhi matakwa ya taarifa ya usanifu iliyoidhinishwa. Katika kaguzi hizo masuala mbalimbali yalibainika ikiwemo kukosekana kwa visima vya kufuatilia uwepo wa nyufa zinazovujisha maji kutoka katika bwawa la topetaka (monitoring boreholes) na wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo.

***100. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya migodi saba (7) ya uchimbaji madini iliwasilisha maombi ya uidhinishaji wa mifumo ya kupandisha na kushusha watu na mizigo mgodini *(Hoisting Systems)* ambapo mifumo hiyo ilikaguliwa. Ukaguzi ulilenga kuhakikisha kama mifumo hiyo imekidhi vigezo stahiki ili iweze kupata idhini ya matumizi kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Migodi. Katika kaguzi hizo mapungufu kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na kutumia vifaa visivyo na ubora na wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo.

***101. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, mitambo 52 ya kuchenjulia dhahabu ya *CIP/CIL; Vat Leaching* 509 na *Elution* 204 zilikaguliwa katika Mikoa ya Kimadini 25. Kaguzi hizi zililenga kuhakikisha miradi inakidhi matakwa ya sheria na taratibu ambazo zimeainishwa katika Sheria ya Madini Sura 123. Miongoni mwa masuala yaliyobainika ni pamoja na maeneo yenye marudio kutowekewa mifereji/kuta ya

kuyazunguka kwa lengo la kuzuia utitirishaji wa maji kwenda kwenye mazingira. Wahusika walirekebisha mapungufu hayo kama walivyoelekezwa.

***102. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, mipango ya ufungaji migodi minne (4) ilijadiliwa na Kamati ya Kitaifa ya Ufungaji Migodi. Kati ya mipango hiyo, hakuna mpango ulioidhinishwa kutokana na mapungufu mbalimbali yaliyobainika ikiwemo kukosekana kwa taarifa za utafiti wa uimara wa miamba (Geotechnical studies), jiokemia, hydrolojia, pamoja na kukosekana kwa maoni ya wadau wa Kamati ya Wilaya ya Ufungaji Migodi (District Mine Closure Committee - DMCC) ili kuainisha miradi ya kiuchumi kwa jamii baada ya maisha ya mgodi. Wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo.

***103. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, elimu kuhusu masuala ya usalama, afya, mazingira pamoja na usimamizi na matumizi ya baruti ilitolewa kwa wachimbaji wadogo wa madini katika mikoa ya kimadini 23 ambapo jumla ya wachimbaji wadogo na wadau wa madini 18,621 walishiriki mafunzo hayo.

### (iv) Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini (Local Content) na Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (CSR)

***104. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya mipango 1,082 ya Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini iliwasilishwa kati ya mipango 750 iliyopangwa kuwasilishwa kwa kipindi husika. Aidha, Mipango 1,081 iliidhinishwa na mpango mmoja (1) haukuidhinishwa kutokana na kutokidhi matakwa ya kisheria. Kati ya mipango 1,082 iliyowasilishwa, 13 ilihusisha leseni za uchimbaji mkubwa (SML), 15 leseni za uchimbaji wa kati (ML), 11 leseni za uchimbaji mdogo (PML), 31 leseni za utafutaji (PL) na 1,012 ni watoa huduma mbalimbali kwa wamiliki wa leseni za madini. Katika kutekeleza matakwa ya Kanuni za *Local Content*, Tume ya Madini ilitangaza huduma na bidhaa 20 ambazo zinapaswa kutolewa na watanzania au kampuni zinazomilikiwa na watanzania.

***105. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2026, jumla ya ajira 20,421 zilizalishwa katika migodi mbalimbali. Kati ya ajira hizo, watanzania ni 19,695 na wageni 726. Aidha, kampuni za madini na watoa huduma zilinunua bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi 4,007,548,722,894.90 kutoka kampuni za Kitanzania sawa na asilimia 90.18 ya ununuzi wote wenye thamani ya shilingi

4,443,900,487,725.71. Vilevile, kupitia CSR miradi yenye thamani ya shilingi 16,173,999,085.52 ilitekelezwa katika Mikoa ya Kimadini ya Kahama, Mara, Geita, Songwe, Singida, Dar es Salaam, Lindi, Mwanza na Shinyanga. Miradi hiyo ilihusisha masuala ya afya, kilimo, michezo, miundombinu ya barabara, mazingira na elimu.

**(v) Huduma za Maabara**

***106. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya sampuli 8,629 za wateja mbalimbali zilipokelewa na kuchunguzwa kupitia maabara ya Tume ya Madini. Kati ya sampuli hizo, 2,696 zilitoka migodi mikubwa ya dhahabu kwa ajili ya kuwezesha Serikali kukokotoa mapato stahiki na 5,933 zilitoka kwa wateja binafsi ili kuwasaidia kufanya maamuzi sahihi katika uzalishaji na biashara ya madini. Huduma iliyotolewa iliwezesha Serikali kukusanya shilingi 308,972,000.00.

**(vi) Ukaguzi wa Hesabu za Fedha na Kodi**

***107. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, ukaguzi ulifanyika katika migodi ya kati na mikubwa pamoja na miradi ya ujenzi wa barabara ambapo masuala mbalimbali yalibainika kutokana na kaguzi hizo ikiwa ni pamoja na hoja za mapunjo ya mrabaha na ada ya ukaguzi zenye jumla ya shilingi 2,459,084,728.94 ikijumuisha shilingi 1,843,925,731.91

ikiwa ni mapunjo ya mrabaha; shilingi 555,158,997.03 ni ada ya ukaguzi; na shilingi 60,000,000.00 ni adhabu kwa kukiuka Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania za Mwaka 2018.

***108. Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ukaguzi uliofanyika mwaka 2025/2026, jumla ya shilingi 2,699,419,438.66 zimekusanywa katika kipindi rejewa. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,968,667,252.96 ni mrabaha, shilingi 540,752,185.70 ni ada ya ukaguzi na shilingi 190,000,000.00 ni adhabu kwa ukiukwaji wa Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania.

### b. TAASISI YA JIOLOJIA NA UTAFITI WA MADINI TANZANIA (GST)

***109. Mheshimiwa Spika,*** jukumu la Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania ni kufanya tafiti za jiosayansi kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini. Kupitia tafiti hizo taarifa mbalimbali za jiosayansi za uwepo wa madini nchini huandaliwa ili kuvutia uwekezaji katika utafutaji wa madini wa kina kwa lengo la kuanzisha migodi mipya.

***110. Mheshimiwa Spika,*** taarifa hizo za jiosayansi hutumika katika sekta nyingine za kiuchumi kama vile kilimo, maji na ujenzi. Pia, GST ina jukumu la ufuatiliaji wa majanga ya asili ya jiolojia ikiwemo matetemeko ya ardhi,

milipuko ya volkano na maporomoko ya ardhi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, GST imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

### (i) Tafiti za Jiosayansi na Uboreshaji wa Kanzidata ya Taifa ya Taarifa za Miamba na Madini

***111. Mheshimiwa Spika,*** GST imekamilisha kuchora ramani mbili (2) za jiolojia na kuandaa ripoti zake baada ya kufanya ugani wa jiolojia katika QDS 221 na 222. QDS hizo zipo katika Wilaya za Kibiti na Rufiji katika Mkoa wa Pwani. Aidha, matokeo ya ugani huo yalionesha uwepo wa madini ya chokaa na miamba yenye ubora wa kuzalisha kokoto. Vilevile, GST ilifanya utafiti kuhusu kutambua umri wa miamba aina ya *granitoids* katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria. Taarifa kuhusu umri wa miamba itasaidia kubaini maeneo yenye madini na itachapishwa kwenye majarida yenye kutambulika.

***"Natoa wito kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kutumia taarifa hizo kuweza kufanya uwekezaji katika maeneo husika"***

***112. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, GST imetoa ushauri elekezi kwa wadau 49 waliowasilisha maombi katika nyanja za utafiti na uchenjuaji madini kwa Taasisi za Serikali na binafsi,

kampuni za uchimbaji wa kati na mkubwa pamoja na wachimbaji wadogo. Aidha, ushauri wa kitalaam ikiwa ni pamoja na kubainisha mwelekeo wa mbale zinazobeba madini na namna bora ya uchenjuaji ulitolewa kwa wachimbaji wadogo 42 na utafiti kwa wachimbaji wakubwa wawili (2). Vilevile, ushauri ulitolewa kwenye maeneo ya ujenzi wa miundombinu hasa majengo kwa Taasisi nne (4) za Serikali na Taasisi binafsi moja (1).

***113. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika GST ilifanya utafiti maalumu ili kubaini maeneo yenye nyufa hai (active fault zone) zinazoweza kuwa hatarishi kutokana na matetemeko katika Wilaya ya Hanang Mkoa wa Manyara. Matokeo ya utafiti huo yaliainisha maeneo yaliyo salama na kubainisha viashiria hatarishi kwa makazi. Taarifa hiyo iliwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Kitengo cha Maafa.

***114. Mheshimiwa Spika,*** GST inaendelea na ukamilishaji wa taratibu za ununuzi wa helikopta. Kwa sasa inafanya majadiliano na mzabuni aliyepatikana kabla ya kuingia kwenye mkataba wa ununuzi. Helikopta hii itasaidia kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia (High Resolution Airborne Geophysical Survey) katika maeneo mbalimbali nchini.

***115. Mheshimiwa Spika,*** GST imeendelea kujenga Mfumo wa Utunzaji na Usambazaji wa Taarifa za Jiosayansi na Rasilimali Madini ambapo hadi kufikia Machi 2026 ujenzi umefikia asilimia 45. Aidha, kukamilika kwa mfumo huo utaongeza usalama wa kanzidata ya taarifa za madini na utarahisisha utunzaji na usambazaji wa taarifa hizo kwa wadau.

**(ii) Uboreshaji wa Huduma za Maabara**

***116. Mheshimiwa Spika,*** maabara ya GST ni mojawapo ya maabara za jiosayansi inayofanya uchunguzi kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika kimataifa na ina Ithibati ya ubora (ISO 17025:2017). Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, GST imeanza ujenzi wa maabara ya kisasa (State-of-the-Art Laboratory) Mkoa wa Dodoma ambapo hadi sasa umefikia asilimia 8.5. Aidha, ujenzi wa maabara hiyo unatarajia kuongeza uwezo wake wa kufanya uchunguzi wa aina nyingi za madini ikiwemo ya kimkakati ambayo kwa sasa baadhi yanapelekwa nje ya nchi kufanyiwa uchunguzi.

***117. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, maabara ya GST imefanyiwa ukaguzi na Shirika linalodhibiti ubora wa huduma za maabara katika nchi zilizopo Kusini mwa Bara la Afrika (Southern African Development Community Accreditation Services - SADCAS) tarehe 24 Februari,

2026. Kupitia ukaguzi huo, maabara ya GST imekidhi vigezo vya kuendelea kuwa na Ithibati ya uchunguzi wa madini. Hii inawezesha majibu yanayotolewa na maabara ya GST kuendelea kutambulika Kimataifa.

***118. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika jumla ya sampuli 16,612 zimefanyiwa uchunguzi wa jiokemia, *geotechnical*, majaribio ya uchenjuaji madini pamoja na utambuzi wa vito na madini yanayounda miamba (Petrographic Study) katika maabara ya GST.

***119. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, GST imefanya utafiti maalum wa udongo mfinyanzi (Ball Clay) katika Mkoa wa Dodoma Wilaya za Bahi, Mpwapwa, Chamwino na Dodoma Mjini. Utafiti huo ulilenga kubainisha maeneo yanayoweza kuwa na malighafi ya kutosha na kufaa kutengeneza vyungu vya kuyeyushia sampuli za miamba au udongo wenye madini ya metali husuan dhahabu. Lengo la utafiti huo ni kuiwezesha GST kupata maeneo yenye uhakika wa madini hayo na kuzalisha vyungu hivyo.

**(iii) Ufuatiliaji wa Majanga ya Asili ya Jiolojia na Uelimishaji wa Umma Kuhusu Namna Bora ya Kupunguza Athari za Majanga**

***120. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, GST kwa kushirikiana na wataalamu

kutoka Chuo Kikuu cha Goethe cha Ujerumani ilifanya ufuatiliaji wa kina kuhusu mitetemo katika Mlima Oldoinyo Lengai ambapo vifaa 32 vya kupima mitetemo vilisimikwa katika eneo la mlima huo. Usimikaji wa vifaa hivyo utasaidia kutambua mwenendo wa mabadiliko yanayotokea.

### c. SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA (STAMICO)

***121. Mheshimiwa Spika,*** STAMICO imepewa dhamana ya kuwekeza katika miradi ya kimkakati kwenye Sekta ya Madini kwa niaba ya Serikali. Aidha, Shirika limepewa jukumu la kuratibu uendelezaji wa wachimbaji wadogo nchini kwa kutoa ushauri wa kitaalamu. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, STAMICO imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

#### (i) Uimarishaji wa Ukusanyaji wa Mapato

***122. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 STAMICO ilipanga kukusanya shilingi 201,883,018,735.00. Hadi kufikia Machi 2026, shilingi 60,043,431,896.00 zilikusanywa sawa na asilimia 40 ya lengo la makusanyo kwa kipindi rejewa. Lengo hilo halikufikiwa na STAMICO kutokana na kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa mikataba ya huduma ya uchorongaji; kushuka kwa bei ya makaa ya mawe kwenye soko la dunia; na Shirika kuchelewa kupokea mitambo ya

kuzalisha nishati safi ya *Rafiki Briquettes* kutoka nje ya nchi.

- **Uzalishaji wa Makaa ya Mawe na Nishati Mbadala (Rafiki Briquettes)**

***123. Mheshimiwa Spika,*** STAMICO imeendelea na uzalishaji wa makaa ya mawe kupitia mradi wa Kiwira-Kabulo ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya tani 214,354 zimezalishwa. Kati ya kiasi hicho, tani 141,453 zimeuzwa na kuliingizia Shirika shilingi 6,207,291,139.00 na shilingi 1,626,764,661.62 zimelipwa kama mrabaha, ada ya ukaguzi, ada ya usafirishaji nje ya nchi (export fee) na ushuru wa huduma.

***124. Mheshimiwa Spika,*** Shirika kupitia mradi wa makaa ya mawe wa Kiwira - Kabulo umetekeleza shughuli za CSR ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 mradi huo umechangia shilingi 75,600,300.00 katika ujenzi wa madarasa matatu (3) katika Shule ya Msingi Kapeta, Wilaya ya Ileje – Mkoa wa Songwe.

***125. Mheshimiwa Spika,*** Shirika linaendelea na uzalishaji wa nishati safi ya Rafiki *Briquettes*. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Shirika limefanikiwa kuzalisha tani 1,530 za Rafiki *Briquettes* zenye thamani ya shilingi 1,460,738,800.00. Shirika limekamilisha usimikaji wa mitambo miwili (2) katika Mikoa ya Dodoma na Tabora.

Kiwanda cha Tabora kilizinduliwa tarehe 21 Februari, 2026. Aidha, Kiwanda cha Dodoma kinatarajiwa kuzinduliwa mwezi Mei, 2026.



**Picha Na. 8:** *Kiwanda cha kuzalisha Nishati Safi ya Rafiki Briquettes Mkoani Tabora ambacho kilizinduliwa tarehe 21 Februari, 2026.*

***126. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa masoko, Shirika linaendelea kuitangaza nishati hiyo katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuweza kupata masoko zaidi. Juhudi hizo zimewezesha taasisi na maeneo mbalimbali kuanza kutumia nishati safi ya Rafiki *Briquette* ikiwa ni pamoja na Jeshi la Wananchi (JWTZ), Jeshi la Magereza, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Taasisi za Elimu (Shule na Vyuo), VETA, Soko la Samaki Feri, Soko la Kuchoma Nyama Kumbi la Moto na Zanzibar kupitia

wakala wa Kikundi cha Maisha *Game*. Aidha, Shirika linauza bidhaa hiyo kupitia mawakala ambao wengi wao ni vikundi vya wanawake ikiwemo kikundi cha "Wanawake na Samia" waliopo kila Mkoa.

- **Shughuli za Uchorongaji**

***127. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Shirika limeendelea kufanya kandarasi katika migodi ya dhahabu ya GGM, Buckreef na Shanta (Singida na Chunya). Vilevile, Shirika limefanikiwa kupata kandarasi mpya kwa kampuni ya *Buhemba Resources* na kampuni ya GFX. Kandarasi hizi zimeiongezea Shirika shughuli za uchorongaji na uwezo wa ukusanyaji wa mapato. Jumla ya mita 86,037.64 zilichorongwa katika miradi hiyo. Kutokana na shughuli za uchorongaji huo, Shirika limekusanya jumla ya shilingi 38,374,171,624.00.

- **Uzalishaji wa Kokoto – Chigongwe**

***128. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya tani 5,475 za kokoto zimezalishwa na kuuzwa ambapo Shirika limepata mapato ya shilingi 346,399,600.00. Kutokana na mauzo hayo Shirika liliweza kulipa Serikalini shilingi 13,659,984.00 kama mrabaha na tozo mbalimbali.

### (ii) Uendelezaji wa Leseni za Shirika

***129. Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kuendeleza leseni zake kwa kufanya utafiti lenyewe na kwa njia ya ubia. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Shirika limefanya utafiti wa madini ya dhahabu, kinywe, *lithium*, *phosphate* na bati (tin) katika leseni zake zilizopo kwenye Hifadhi ya Kigosi Wilaya ya Bukombe - Geita, Wilaya ya Ruangwa na Nachingwea - Lindi, Wilaya ya Bahi - Dodoma na Wilaya ya Kyerwa - Kagera.

***130. Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza leseni za shirika, kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Shirika limesaini mikataba miwili (2) ya ubia kuendeleza leseni za utafiti wa madini ya dhahabu na kinywe. Kwa madini ya dhahabu, Shirika limesaini mkataba na Kampuni ya *Plantcor Mining and Plant Hire* (PTY) Ltd ya nchini Afrika Kusini tarehe 24 Februari 2026 kwa kuendeleza leseni zilizopo Kigosi mkoani Geita. Kufuatia kusainiwa kwa mkataba wa ubia, taratibu za kutafuta wakandarasi wa utafiti wa kijiofizikia na kijiokemia zinaendelea. Kwa upande wa madini ya kinywe, Shirika limesaini Mkataba na Kampuni ya *Planet One Natural Resources Holdings PTE Limited* ya nchini Singapore tarehe 30 Machi 2026 wa kuendeleza leseni zake za utafiti zilizopo Mirerani, Manyara. Vilevile, Shirika limesaini Mkataba na kampuni

ya *Costal Nickel* ya nchini China tarehe 12 Septemba 2025 wa kuchimba madini ya Nikeli katika eneo la Ntaka Lindi.




**Picha Na. 9:** *Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa (Mb.), Naibu Waziri wa Madini akishuhudia utiaji saini wa mkataba kati ya STAMICO na Kampuni ya "Plantcor Mining and Plant Hire (PTY) Ltd" kwa ajili ya uendelezaji wa leseni za shirika katika eneo la Kigosi.*

### (iii) Utekelezaji wa Miradi ya Ubia na Kampuni Tanzu

- **Mgodi wa Dhahabu wa Biharamulo (Kampuni Tanzu ya STAMIGOLD)**

***131. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, mgodi wa STAMIGOLD umezalisha dhahabu wakia 7,530.98 na wakia 486.00 za madini ya fedha na kupata shilingi 78,530,155,276.44. Aidha,

kutokana na mauzo hayo, mgodi umelipa shilingi 3,337,531,599.25 kama mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa huduma. Vilevile, mgodi umenunua mitambo ya uchimbaji yenye thamani ya shilingi 5,440,000,000.00 ambayo ni *Excavators* 2, *Tipper Trucks* 6, *Water Bowser* 1 na *Wheel Loader* 2.

***132. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, uchunguzi wa uimara wa miamba (geotechnical investigation) ulifanyika kwa ajili ya kubaini usalama wa mgodi wa chini ya ardhi. Vilevile, STAMIGOLD imekamilisha utafiti wa mashapo ulioanza mwaka 2022/2023. Pia, mgodi unaendelea kufanya uhakiki wa mashapo mengine kwenye leseni Na. SML157/2003 na PL 13075/2024 kwa kutumia teknolojia mbalimbali za utafiti. Lengo la uhakiki huo ni kuiwezesha STAMIGOLD kubaini mashapo mapya. Matokeo ya awali yanaonesha uwepo wa wakia za dhahabu 196,990 ndani ya SML 157/2003 na viashiria vya uwepo wa wakia za dhahabu 105,000 kwenye leseni Na. PL 13075/2024. Hatua hii imelenga kuongeza uhai wa mgodi.

***133. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, mgodi unatekeleza miradi ya wajibu wa mmiliki wa leseni kwa jamii (CSR) kiasi cha shilingi 94,960,465.00 Wilayani Biharamulo katika ujenzi wa bweni la Shule ya Msingi Iyengamulilo B' Kata ya Nyantakara;

darasa moja (1) katika shule ya Msingi Midaho, Kata ya Lusahunga; darasa moja (1) katika Shule ya Msingi Kisuno, Kata ya Bisibo; na ujenzi wa matundu nane (8) ya vyoo katika Shule ya Msingi Mafukwe, Kata ya Kabindi.

- **Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza (Kampuni ya Ubia Mwanza Precious Metals Refinery)**

***134. Mheshimiwa Spika,*** kiwanda cha kusafisha dhahabu Mwanza kinamilikiwa na STAMICO kwa asilimia 25 na mbia asilimia 75. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kiwanda kimenunua dhahabu ghafi tani 1.960 yenye thamani ya shilingi 580,256,753,948.30 na kulipa Serikalini shilingi 24,660,912,042.80 ikiwa ni mrabaha na ushuru wa huduma. Aidha, kiwanda kimetoa huduma za usafishaji dhahabu jumla ya tani 6.217 kwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) pamoja na wateja wengine (dealers) kwa gharama ya shilingi 2,490,913,950.36. Kiwanda kimeendelea kupokea dhahabu inayonunuliwa na BoT kutoka kwa wachimbaji pamoja na wafanyabiashara wa madini kwa ajili ya kuisafisha kwa kiwango cha asilimia 99.99.

***135. Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha kiwanda kupata dhahabu ya kutosha, Shirika limefanya uhamasishaji kwa wachimbaji wadogo waweze kusafisha dhahabu kwenye

Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza. Uhamasishaji huo ulihusu kuwapatia elimu ya manufaa yatokanayo na usafishaji dhahabu kwenye *refinery* ikiwa ni pamoja na kupata faida itokanayo na punguzo la mrabaha kwenye viwanda vya usafishaji dhahabu ndani ya nchi.

- **Mgodi wa Dhahabu wa Buckreef (Kampuni ya Ubia ya Buckreef Gold Company)**

***136. Mheshimiwa Spika,*** mgodi wa dhahabu wa Buckreef uliopo mkoani Geita unamilikiwa kwa ubia kati ya STAMICO yenye hisa asilimia 45 na kampuni ya TRX Gold Tanzania yenye hisa asilimia 55. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, mgodi umezalisha wakia za dhahabu 18,241.52 zenye thamani ya shilingi 194,232,491,026.87 na kulipa Serikalini shilingi 12,851,094,727.87 ikiwa ni mrabaha, ada ya ukaguzi, ushuru wa huduma na *HIV response levy*.

***137. Mheshimiwa Spika,*** mgodi wa Buckreef umetekeleza shughuli za CSR ambapo katika kipindi husika umetoa shilingi 172,196,260.18 katika kuboresha miundombinu na ujenzi wa nyumba za watumishi katika kituo cha afya Butundwe, ukarabati wa barabara ya kijiji cha Mnekezi na uchimbaji wa visima vya maji safi katika kijiji cha Lubanda na Lwamgasa Wilaya ya Geita.

- **Mgodi wa Nikeli – Ntaka (Kampuni ya Ubia Coastal Nickel Industry Limited)**

***138. Mheshimiwa Spika,*** mgodi wa uchimbaji madini ya nikeli uliopo Ntaka Mkoa wa Lindi unamilikiwa kwa ubia wa asilimia 15 kwenye mapato ghafi kwa STAMICO na *Coastal Nickel Industry Limited*. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, tani 4,973 za nikeli zinazokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi 12,912,364,398 zimechimbwa. Shirika linatarajia kupata takriban shilingi 1,936,854,660.00 kama mapato yatokanayo na umiliki wake.

**(iv) Shughuli za Uchimbaji Mdogo na Uimarishaji wa Vituo vya Mfano**

***139. Mheshimiwa Spika,*** STAMICO inaendelea kuratibu shughuli za uchimbaji mdogo kwa kutoa huduma za kitaalam kwa Wachimbaji Wadogo katika nyanja za utafiti, uchimbaji, uchenjuaji madini pamoja na utunzaji wa mazingira. Aidha, jumla ya wachimbaji wadogo 451 wamepatiwa mafunzo kupitia vituo vya mfano. Vilevile, kupitia vituo hivyo huduma ya uchenjuaji mbale ya dhahabu kwa wateja 32 ilitolewa ambapo dhahabu ya uzito wa gramu 106,029.18 yenye thamani ya shilingi 29,633,631,202.30 ilichenjuliwa na kuipatia Serikali mapato ya shilingi 2,163,255,077.77.

***140. Mheshimiwa Spika***, STAMICO imeendelea kutoa huduma ya uchorongaji kwa bei nafuu kwa wachimbaji wadogo ambapo katika kipindi rejewa, wachimbaji wadogo wamepata huduma hiyo katika maeneo ya Mbangala – Songwe, Sambaru – Singida, Mwagiwagi – Masumbwe, Kasimenti – Makongolosi, Kerende na Nyamongo – Tarime, Mnyolima - Mbeya, Melela – Morogoro, Kondoa – Dodoma, Isaula, Itumbi na Mapogoro – Chunya na Lwamgasa – Geita. Jumla ya mita 3,896.59 zimechorongwa katika maeneo hayo.

***141. Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza wigo wa kuwahudumia wachimbaji wadogo, shirika limenunua vifaa wezeshi vya mitambo ya uchorongaji na mashine 10 za kupunguza ukubwa wa mawe ya mbale (crusher) kwa ajili ya vikundi maalum vya wanawake. Mashine hizo zimegawiwa kwa vikundi vya wanawake katika mikoa ya Iringa, Shinyanga, Dar es Salaam, Geita, Simiyu, Ruvuma na Mwanza. Aidha, jitihada zinaendelea kufanyika ili kupata mashine nyingine kwa vikundi vya wanawake katika mikoa mingine.

***142. Mheshimiwa Spika***, katika zoezi la kuwaendeleza wazalishaji wadogo wa chumvi, Shirika linaendelea na ujenzi wa kiwanda cha kusafisha chumvi katika eneo la Nangurukuru kilichopo Wilaya ya Kilwa - mkoani Lindi. Aidha, hadi kufikia Machi 2026 ujenzi wa jengo la kiwanda

umekamalika. Hatua inayoendelea ni usimikaji wa mitambo ya kusafisha chumvi.

### d. KITUO CHA JEMOLOJIA TANZANIA (TGC)

***143. Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Jemolojia Tanzania kinatoa mafunzo ya uongezaji thamani madini ngazi ya astashahada na stashahada katika fani za utambuzi wa madini ya vito; uchongaji wa bidhaa za mapambo na urembo zinazotokana na miamba; ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito na utengenezaji wa bidhaa za usonara. Aidha, TGC inatoa huduma za utambuzi wa madini ya vito kupitia maabara yake na utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na madini ya vito na miamba. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 TGC imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

#### (i) Utoaji wa Mafunzo na Huduma Nyingine

***144. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya wanafunzi 93 walidahiliwa kati ya hao wanafunzi 35 ngazi ya Astashahada (*NTA Level* 4) na wanafunzi 58 ngazi ya Stashahada (*NTA Level* 5 na 6). Aidha, Kituo kilidahili wanafunzi 27 wa kozi za muda mfupi katika fani za ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito *(Lapidary),* usonara (*jewellery*) na sayansi ya madini ya vito (*Gemology)*. Kituo kilikusanya shilingi 88,743,077.00

ikiwa ni malipo ya ada na michango mingine inayotokana na mafunzo.

***145. Mheshimiwa Spika,*** ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soko, TGC iliandaa mitaala miwili (2) katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ya mafunzo ya jemolojia na usonara (gemstone jewellery technology and gemstone technology - NTA Level 4, 5 and 6). Aidha, mitaala hiyo iliidhinishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) na kuanza kutumika katika Mwaka wa Masomo 2025/2026.

***146. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, *Sunset Gems Ltd* ilitoa mafunzo kwa watumishi na wanafunzi wa TGC kuhusu utumiaji wa mashine za kukata vito kutoka nchini Thailand ikiwa ni utekelezaji wa makubaliano ya pamoja (MOU). Pia, Taasisi ya *United African University of Rwanda* (UAUR) ya nchini Rwanda ilitoa mafunzo ya Jemolojia kwa watumishi na wanafunzi wa TGC.

***147. Mheshimiwa Spika,*** TGC imeendelea kutoa huduma mbalimbali kwa wadau ikiwa ni pamoja na kufanya utambuzi wa madini ya vito, ukataji wa madini ya vito na utengenezaji wa bidhaa za usonara. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya sampuli za madini ya vito 714 zilipokelewa na kutolewa taarifa za utambuzi.

Aidha, huduma ya utengenezaji wa bidhaa za usonara 42 zilitolewa. Kutokana na huduma hizo, shilingi 20,856,000.00 zilipatikana.

**(ii) Uzalishaji wa Bidhaa**

***148. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, TGC imeendelea kufanya shughuli za usanifu na uzalishaji wa bidhaa za madini ikiwa ni pamoja na kutengeneza bidhaa za usonara, kukata vito na uchongaji wa miamba ambapo vito 820 vilikatwa, bidhaa 959 za usonara na urembo za madini ya vito zilizalishwa, bidhaa 5,206 za mapambo na shanga (beads) 6,211 zilitengenezwa kwa kutumia miamba. Kutokana na uzalishaji huo Kituo kilikusanya jumla ya shilingi 73,816,413.14.

***149. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na soko la uhakika la bidhaa zinazozalishwa, TGC imefungua kituo cha mauzo na maonesho ya madini ya vito na bidhaa za usonara katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha – AICC. Vilevile, TGC imeendelea kuimarisha vituo vya mauzo vilivyopo katika eneo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro - KIA na katika Ofisi za TGC.



**Picha Na. 10:** *Kituo cha mauzo na maonesho ya madini ya vito na bidhaa za usonara kilichopo katika Ukumbi wa Mkutano wa AICC.*

## e. TAASISI YA UHAMASISHAJI UWAZI NA UWAJIBIKAJI KATIKA RASILIMALI MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA (TEITI)

***150. Mheshimiwa Spika,*** TEITI ina jukumu la kuhakikisha kuwa mapato yatokanayo na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia yanahakikiwa na kutumika kwa manufaa ya wananchi wote. Aidha, TEITI ina jukumu la kuhakikisha kampuni zinazofanya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia inaweka wazi taarifa za shughuli zao kulingana na Sheria ya TEITA Sura 447. Vilevile, TEITI ina jukumu la kuwajengea uwezo wananchi katika kutumia takwimu

zinazotokana na shughuli za uendeshaji wa makampuni ili kushiriki mijadala kuhusu manufaa ya uchimbaji madini, mafuta na gesi asilia. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, TEITI imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

**(i) Uandaaji na Uwekaji Wazi Ripoti ya 16 ya TEITI kwa Mwaka 2023/2024**

***151. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya TEITI inaendelea na ukamilishaji wa ripoti ya 16 inayoonesha ulinganishi wa malipo ya kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kampuni zilizochaguliwa kwa ajili ya zoezi la ulinganishi ni kampuni 37 zinazojihusisha na shughuli za madini, mafuta na gesi asilia. Aidha, ripoti hiyo itahusisha kampuni zilizolipa kodi na tozo mbalimbali Serikalini kuanzia shilingi bilioni mbili. Ripoti hii itawekwa wazi kwa umma ifikapo Juni, 2026.

**(ii) Uwekaji Wazi Mikataba ya Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia**

***152. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa TEITI imeweka wazi taarifa tatu (3) za mikataba ya kampuni za uchimbaji madini ambazo ni *Tembo Nickel Corporation Limited, Faru Graphite Corporation Limited* na *Williamson Diamond Limited*. Utekelezaji wa takwa hili ni kwa mujibu

wa vigezo vya kimataifa vya uwazi na uwajibikaji (*EITI Standard, 2023*) pamoja na Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia, Sura 447. Aidha, TEITI inaendelea kushirikiana na wadau wengine wa mikataba ya madini, mafuta na gesi asilia katika kuhakikisha kuwa taarifa za mikataba yao inawekwa wazi kwa umma kwa mujibu wa sheria.

**(iii) Utoaji Elimu Kwa Umma Kuhusu Matumizi ya Takwimu za Ripoti ya TEITI**

***153. Mheshimiwa Spika,*** TEITI imeendelea kuelimisha Umma kuhusu matumizi ya takwimu zinazotolewa kwenye ripoti zake kupitia warsha, runinga (TBC, ITV, AZAM, Clouds na Channel Ten), redio, tovuti, mitandao ya kijamii na kwenye maonesho mbalimbali ikiwemo Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba na Maonesho ya Nane ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini. Aidha, TEITI ilifanya warsha katika Mkoa wa Mtwara ambapo washiriki wakiwemo Viongozi wa Halmashauri, Madiwani wa Mikoa ya Mtwara na Lindi na Viongozi wa Halmashauri walipewa elimu ya namna ya kutumia takwimu zinazotolewa na ripoti za TEITI.



**Picha Na. 11:**: *Bi. Mariam Mgaya, Katibu Mtendaji wa TEITI (wa pili kulia) akiuelimisha Umma kuhusu majukumu ya TEITI kupitia kipindi cha "Morning Trumpet", Azam TV.*

### (iv) Ukamilishaji wa Mfumo wa Kielektroniki Utakaotumika Kuandaa Taarifa za TEITI

***154. Mheshimiwa Spika,*** mfumo wa kielektroniki utakaotumika kuandaa taarifa za TEITI za kila mwaka ujulikanao kama "*Extractive Data Reporting Management Information System (EDR-MIS)*" umekamilika na kuwa tayari kutumika. Mfumo huu utatumika kukusanya na kuchakata takwimu mbalimbali kutoka katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia pamoja na Taasisi za Serikali ambazo zitawezesha kuandaa taarifa za TEITI. Matumizi ya mfumo huu utarahisisha uaandaji wa taarifa za TEITI.

### (v) Kufanya Tafiti Mbalimbali za Namna Wananchi Watakavyonufaika na Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia

***155. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, TEITI imekamilisha utafiti kuhusu utekelezaji wa sheria katika eneo la Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini (Local Content) na Wajibu wa Kampuni za Madini kwa Jamii (Corporate Social Responsibility) uliofanyika kwa kampuni za madini zenye leseni za uchimbaji wa kati na mkubwa katika mikoa ya Geita na Mara. Matokeo ya utafiti huo ni: kuwepo kwa maendeleo katika utekelezaji wa masuala ya *Local Content* na CSR; kutofautiana kwa mitazamo katika kupanga vipaumbele vya utekelezaji wa miradi ya CSR; uelewa na ushirikishwaji mdogo wa wadau; uwezo mdogo na kukosa uadilifu kwa baadhi ya wazabuni. Aidha, Wizara kupitia TEITI inaendelea kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyobainishwa kwenye taarifa ya utafiti. Vilevile, TEITI inaendelea na maandalizi ya kufanya tafiti kwa upande wa Sekta ya Uziduaji katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

## D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

***156. Mheshimiwa Spika,*** katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara imezingatia miongozo ifuatayo: Mwongozo wa Kitaifa wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2026/2027; Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 – 2030/2031 (FYDP IV); DIRA 2050; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Muda Mrefu (LTPP 2050); Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi; Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; *Africa Mining Vision*; Sera ya Madini ya Mwaka 2009; Mpango Mkakati wa Wizara; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Kifungu cha 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439; Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine wa kitaifa pamoja na Maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambayo yaliyotolewa kwa nyakati tofauti.

### I. Vipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

***157. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara ya Madini itatekeleza vipaumbele vifuatavyo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli; kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuendeleza

mnyororo wa thamani katika madini muhimu na madini mkakati; kuhamasisha uwekezaji katika uongezaji thamani madini; kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito; kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za kina za madini; kurasimisha na kuendeleza wachimbaji wadogo na kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya wizara ya madini.

**(i) Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli**

***158. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa uchimbaji wa madini ili uweze kunufaisha nchi na wawekezaji; kuimarisha na kusimamia masoko na vituo vya ununuzi wa madini nchini; na kuendeleza mikakati ya kuimarisha usimamizi wa madini ujenzi na viwandani, soko la tanzanite na madini mengine ya vito hapa nchini ili kuongeza mapato yatokanayo na madini hayo.

***159. Mheshimiwa Spika***, Wizara inatarajia kununua magari kwa ajili ya kuimarisha shughuli za ukusanyaji wa maduhuli. Hatua hii itachangia katika kusimamia ukusanyaji wa maduhuli, udhibiti wa utoroshwaji na biashara haramu ya madini pamoja na kufuatilia shughuli mbalimbali za madini.

***160. Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hayo, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ya kuimarisha utekelezaji

wa Sheria ya Madini, ikiwemo kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini.

***161. Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuimarisha udhibiti na kuzuia utoroshaji wa madini ya tanzanite, katika mwaka ujao wa fedha Wizara kupitia Tume ya Madini, itakamilisha ununuzi wa kofia zenye kamera maalum kwa ajili ya ukaguzi na itahakikisha wakaguzi na wathaminishaji wa madini hayo wanavaa kofia ili kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mwenendo wa uzalishaji na biashara ya madini kwenye Eneo Tengefu la Mirerani.

**(ii) Kuongeza Mchango wa Sekta ya Madini Kwenye Pato la Taifa**

***162. Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza mchango wa wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo: kuhamasisha shughuli za utafiti wa madini na uanzishaji wa migodi mipya, kuimarisha usimamizi wa migodi ya uchimbaji; kuboresha mfumo wa usimamizi wa madini ya ujenzi na ya viwandani; kusimamia utekelezaji wa Sheria inayoitaka migodi mikubwa kuajiri, kununua huduma na bidhaa kutoka hapa nchini na kuhamasisha ushiriki wa Watanzania katika mnyororo wa uchumi wa madini;na kuendelea kuimarisha mazingira wezeshi ya kisera na kisheria. Aidha,

Wizara itahakikisha kuwa wawekezaji waliopewa leseni za uchimbaji wa madini wanaanza uzalishaji mara baada ya kukamilisha taratibu za matakwa ya kisheria.

**(iii) Kuendeleza Mnyororo wa Thamani Katika Madini Muhimu na Madini Mkakati**

***163. Mheshimiwa Spika,*** madini muhimu na madini mkakati ni madini ambayo yana mahitaji makubwa kwenye maendeleo ya uchumi na ulinzi wa Taifa. Madini hayo ni pamoja na *lithium*, *graphite*, *helium, nickel, cobalt, titanium*, *copper, aluminium, niobium* na *rare earth elements* ambayo yanatumika kutengeneza vifaa vya teknolojia ya kisasa ikiwemo nishati safi.

***164. Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza manufaa yatokanayo na madini muhimu na madini mkakati kwa uchumi wa Taifa, Wizara imepanga kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini hayo kwa kufanya yafuatayo: kuhamasisha uwekezaji katika utafutaji na uchimbaji wa madini muhimu na madini mkakati; kufanya utafiti wa mahitaji ya madini mkakati ili kuyafikia masoko mbalimbali duniani; kutoa leseni za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini muhimu na madini mkakati; na kukamilisha na kutekeleza mkakati wa uendelezaji na uvunaji wa madini hayo nchini.

***"Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba watanzania wananufaika ipasavyo na uwepo wa rasilimali za madini muhimu na madini mkakati hapa nchini"***

**(iv) Kuhamasisha Uwekezaji katika Uongezaji Thamani Madini**

***165. Mheshimiwa Spika,*** ili kuhamasisha uwekezaji, Wizara itaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na madini; kuendelea kutoa ushirikiano kwa wamiliki wa viwanda vya usafishaji wa madini ya dhahabu nchini ili kupata ithibati ya LBMA; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Kituo cha Jemolojia Tanzania ili kiweze kutoa mafunzo na huduma kwenye mnyororo wa uongezaji thamani madini kwa ufanisi. Aidha, Wizara itaendelea kutangaza fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye mnyororo wa thamani wa madini nchini kupitia makongamano, maonesho, tovuti na vyombo vya habari.

***166. Mheshimiwa Spika,*** ili kuhamasisha uwekezaji katika uongezaji thamani madini, Serikali imetenga eneo la Buzwagi lililopo Wilaya ya Kahama kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani madini na viwanda vya uzalishaji bidhaa migodini.

***167. Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza kutangaza fursa za uwekezaji nchini, Wizara kwa kushirikiana na Chemba ya Migodi Tanzania (Tanzania Chamber of Mines) itafanya Mkutano wa saba (7) wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini. Mkutano huo unatarajiwa kufanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kuanzia tarehe 19 hadi 21 Novemba, 2026 Jijini Dar es Salaam. Mkutano huu utawakutanisha kwa pamoja makundi mbalimbali ya wataalamu wa masuala ya madini, Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa kampuni za utafiti na uchimbaji wa madini, kampuni za utafiti na uchimbaji wa madini, watoa huduma, wafanyabiashara na wawekezaji katika Sekta ya Madini kutoka ndani na nje ya nchi yetu.

**(v) Kuimarisha Uendeshaji wa Minada na Maonesho ya Madini ya Vito**

***168. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hiki Wizara itafanya yafuatayo: kuimarisha uendeshaji wa viwanda vya kuongeza thamani madini nchini sambamba na uendelezaji wa minada na maonesho ya madini ya vito ya Arusha (Arusha Gem Fair - AGF) na Minada ya madini ya vito ya kimataifa ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara ya madini ya vito (Gemstone Hub). Aidha, Wizara itaendelea kuratibu utangazaji wa fursa za uwekezaji zilizopo kupitia makongamano, maonesho, tovuti na vyombo vya habari.

### (vi) Kuongeza Uwekezaji kwenye Tafiti za Kina za Madini

***169. Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa shughuli hii, Wizara itafanya tafiti za kina za jiosayansi ikiwemo jiofizikia (High-resolution Airborne Geophysical Survey) ili kuainisha uwepo wa madini mbalimbali yakiwemo madini muhimu na madini mkakati. Aidha, Wizara kupitia GST itaendelea na ujenzi wa mfumo wa kusimamia taarifa za jiosayansi. Vilevile, Wizara itaendelea kushirikisha wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi ili kushirikiana kufanya utafiti wa madini katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuongeza wigo wa utafiti wa kina wa madini nchini.

### (vii) Kuwarasimisha na Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo

***170. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na taratibu za kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kuweka mazingira wezeshi yatakayowahamasisha kufanya uwekezaji; kuendelea kuhamasisha taasisi za kifedha kutoa mikopo ya fedha na vifaa kwa wachimbaji wadogo; kuandaa Mpango wa kuwatambua na kuwaendeleza wachimbaji wadogo nchini kupitia Mfuko wa Dhamana kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha; kuboresha utendaji wa vituo vya mfano ili kuimarisha utoaji wa huduma na mafunzo kwa wachimbaji wadogo; na

kuimarisha huduma za uchorongaji kwa wachimbaji wadogo.

***171. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuimarisha utekelezaji wa mipango ya kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija kwa kuwatengea maeneo na kuwawezesha kupata leseni kwenye maeneo yenye taarifa za msingi za jiolojia kupitia Programu ya MBT; kuchukua hatua za ufutaji wa leseni za utafiti ambazo hazifanyiwi kazi na kuzirejesha Serikalini ili kupangwa vyema na kugaiwa kwa wachimbaji wadogo; kuhamasisha wachimbaji wadogo kushiriki mikutano, maonesho na makongamano mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kujifunza na kutangaza shughuli zao; kuendesha makongamano kwenye mikoa ya kimadini kwa ajili ya kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo na wananchi kwa ujumla kuhusu masuala ya sheria na kanuni mbalimbali za madini zikiwemo za *Local Content*, *CSR*, Haki Madini na Haki Ardhi; na kuhamasisha wachimbaji wadogo kushiriki kwenye minada na maonesho ya madini ya vito nchini ili kupanua wigo wa biashara.

***172. Mheshimiwa Spika***, ili kuwawezesha wachimbaji wadogo waweze kunufaika na rasilimali madini, Serikali itaendelea kuitumia Timu ya Wataalamu wenye uzoefu na masuala ya fedha, madini na sheria kwa ajili ya kutoa mapendekezo ya namna ya kuwawezesha wachimbaji

wadogo kupata mitaji na msaada wa kiufundi. Hatua hii itawawezesha wachimbaji hao kufanya uchimbaji wenye tija na kunufaika zaidi kiuchumi. Aidha, Wizara kupitia STAMICO itaendelea kuwalea na kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kuwajengea vituo vya mfano katika maeneo yenye uchimbaji mdogo.

***173. Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuwahamasisha sekta binafsi iweze kuanzisha vituo vya kuuza na kukodisha vifaa na mashine mbalimbali za kufanyia shughuli za madini kwa lengo la kuwawezesha wachimbaji wadogo kutekeleza shughuli za madini kwa tija ili kuongeza mchango wao katika Pato la Taifa.

### (viii) Kuzijengea Uwezo Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ya Madini

***174. Mheshimiwa Spika,*** ili kuzijengea uwezo taasisi, Wizara itafanya yafuatayo: kuiwezesha Tume ya Madini kupata rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi; kuendelea kuimarisha STAMICO ili ishiriki kikamilifu kwenye uwekezaji wa shughuli za madini.

***175. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuimarisha GST ili iweze kufanya tafiti za jiosayansi kwa lengo la kubaini maeneo mapya yenye uwepo wa madini; kuimarisha TGC ili iweze kusimamia na kuhamasisha

uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini ya vito na metali za thamani; na kuiwezesha TEITI kupata rasilimali mbalimbali ikiwemo vifaa na vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

## II. Maeneo Mengine Yatakayotekelezwa na Wizara katika Mwaka wa Fedha 2026/2027

***176. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itatekeleza maeneo mengine yatakayosaidia kuboresha zaidi ufanisi wa sekta. Utekelezaji huo umejikita zaidi katika kupata taarifa za jiosayansi kwa kufanya tafiti za kina ili kuendana na matarajio ya "***Mining Vision 2030***"; kuendelea na utekelezaji wa ***Programu ya Mining for a Brighter Tomorrow - MBT*** kwa ajili ya kuwainua wachimbaji ikiwemo wanawake, vijana na makundi yenye uhitaji maalum; kuwajengea uwezo Wataalamu kwenye maeneo muhimu katika Sekta ya Madini; kuboresha usimamizi wa shughuli za madini kidigitali (Mineral Trade Digitization); na usimamizi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

### (i) *Mining Vision* 2030: Madini ni Maisha na Utajiri

***177. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini itaendelea na utekelezaji wa "***Mining Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri"*** inayoweka matamanio ya kuwa na usimamizi

thabiti na endelevu wa rasilimali madini ili kukuza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; na kuboresha maisha ya watanzania kupitia shughuli za madini.

***178. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara kupitia GST inatarajia kufanya tafiti za kina za jiosayansi ikiwemo utafiti wa kina wa jiofizikia *(High Resolution Airborne Geophysical Survey)*. Utafiti huo unatarajia kuongeza taarifa za kina za jiofizikia kutoka asilimia 16 ya sasa hadi kufikia asilimia 34. Aidha, katika utekelezaji wa *Mining Vision 2030* Serikali itaendelea na jitihada za tafiti za kina ili angalau kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2030. Taarifa hizi zitaongeza uelewa wa jiolojia ya nchi yetu na hivyo kuvutia na kuboresha mazingira ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuchochea ufungamanishaji na sekta nyingine za kiuchumi hususan Sekta za Viwanda, Kilimo, Ujenzi, Fedha na nyingine zinazotoa huduma kwenye Sekta ya Madini.

***“Mheshimiwa Spika, binafsi nikushukuru wewe na Bunge lako Tukufu kwa kuniunga mkono katika kuhakikisha utafiti wa kina wa madini unafanyika katika nchi yetu kwa kiasi kikubwa”***

### (ii) Programu ya *Mining for a Brighter Tomorrow* – MBT

***179. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini itaendelea kutekeleza Programu ya MBT kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2025 hadi 2030. Programu hii ni ya mageuzi katika Sekta ya Madini ambayo imeanzishwa kwa ajili ya kuboresha ushiriki wa wachimbaji wadogo ikiwemo wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum katika fursa zilizopo kwenye mnyororo wa thamani wa madini.

***180. Mheshimiwa Spika,*** Programu ya MBT inatarajiwa kuwa na matokeo yafuatayo: kuongeza ushiriki wa vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalum kwenye Uchumi jumuishi kupitia Sekta ya Madini na kuwawezesha kupata kipato na kuwaongezea fursa za ajira.

### (iii) Kuwajengea Uwezo Wataalam kwenye Maeneo Muhimu katika Sekta ya Madini

***181. Mheshimiwa Spika,*** ili kukidhi mahitaji ya rasilimali watu katika shughuli za madini na uhitaji wa teknolojia mahsusi katika mnyororo wa thamani wa madini nchini, Wizara imetenga fedha za kuwajengea uwezo wataalam katika Sekta ya Madini kwa kuwasomesha ndani na nje ya nchi kupitia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu. Mafunzo hayo yatajikita zaidi katika fani za ukadiriaji wa mashapo (resource estimation), modeli za kifedha

(financial modelling), ukaguzi wa fedha na rasilimali madini, uthaminishaji wa madini na uongezaji thamani madini ikiwemo madini ya vito, madini muhimu na madini mkakati.

### (iv) Kuboresha Usimamizi wa Shughuli za Madini Kidijitali

***182. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na hatua za ukamilishaji wa ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Sekta ya Madini Kidijitali utakaojulikana kama "*Mineral Sector Management Information System* (MSMIS)". Mfumo huu unalenga kuimarisha usimamizi, uratibu na upatikanaji wa taarifa za Sekta ya Madini kwa kutumia teknolojia za kidijitali, sambamba na jitihada za Serikali za kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za umma. Mfumo huo utaunganishwa na mifumo mingine ya Serikali ili kuongeza ufanisi katika usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za madini na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

### (v) Usimamizi wa Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

***183. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itaendelea kutekeleza yafuatayo: kufuatilia uzingatiwaji wa masuala ya usalama, afya na utunzaji wa mazingira katika maeneo ya migodi na mitambo ya uchenjuaji wa madini nchini; kuratibu tathmini ya kimkakati

ya mazingira ya sekta na kupitia Mpango Kazi wa Mazingira wa Sekta ya Madini 2025 – 2030; kuendeleza kampeni za uhamasishaji na elimu kwa wachimbaji wa madini kuhusu masuala ya usalama, afya na utunzaji wa mazingira; kufuatilia uwekaji dhamana za urejeshaji wa mazingira na maandalizi ya mipango ya ufungaji migodi nchini; na kuendelea kusimamia Sekta ya Madini ipasavyo ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Shughuli za usimamizi na utunzaji wa mazingira zitasimamiwa kwa kuzingatia Nguzo Na. 3 ya DIRA 2050, Sheria ya Madini Sura 123 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191.

***184. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itatekeleza Mpango Kazi wa Mazingira wa Sekta ya Madini 2025 – 2030 (Mineral Sector Environmental Action Plan – MSEAP) ambao unazingatia Mpango Kazi wa Taifa wa Usimamizi wa Mazingira (National Environmental Action Plan - NEAP) na DIRA 2050. Lengo kuu la Mpango huu ni kujumuisha kanuni za Mazingira, Jamii na Utawala Bora (Environmental, Social and Governance - ESG) katika upangaji, usimamizi na uangalizi wa udhibiti wa Sekta ya Madini nchini, ili kuhakikisha kuwa maendeleo ya rasilimali madini yanachangia ukuaji wa uchumi endelevu bila kuathiri usalama wa mazingira na ustawi wa jamii.

## III. Kazi Zitakazotekelezwa na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

### (i) Tume ya Madini

***185. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Tume ya Madini imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

#### a) Utoaji na Ufuatiliaji wa Leseni za Madini

***186. Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha Sekta ya Madini inaendelea kuchangia katika Pato la Taifa ipasavyo, Tume ya Madini itaendelea kutoa leseni kwa ajili ya shughuli mbalimbali za madini na kufuatilia uendelezaji wa leseni hizo. Tume ya Madini itaendelea kusimamia Sheria ya Madini, ikiwemo kusimamisha au kufuta leseni kwa wamiliki ambao watakiuka masharti ya kisheria. Aidha, Tume ya Madini itaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Vilevile, Tume ya Madini itaendelea kufanya uboreshaji wa huduma za utoaji wa leseni ikiwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini.

**b) Kuimarisha Usimamizi wa Shughuli za Madini na Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali**

***187. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini itaendelea kuimarisha usimamizi ili kuhakikisha kwamba migodi mikubwa na ya kati ambayo imepewa leseni inaanza uzalishaji; kuimarisha usimamizi katika masoko ya madini na vituo vya ununuzi wa madini nchini; kuendelea kudhibiti vitendo vya utoroshwaji wa madini nchini; kutanua wigo wa usimamizi wa uzalishaji wa madini ya ujenzi na madini ya viwandani; kuimarisha mifumo ya TEHAMA; kuendelea kufanya tafiti za kuibua vyanzo vipya vya mapato; na kuimarisha ukaguzi wa hesabu za fedha na kodi kwenye Sekta ya Madini ili kuhakikisha kuwa Serikali inapata mapato stahiki.

**c) Kuimarisha Ukaguzi wa Afya, Usalama, Mazingira na Uzalishaji wa Madini**

***188. Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kunakuwa na shughuli za uchimbaji madini endelevu, Tume ya Madini itaendelea kufanya kaguzi za usalama, afya na mazingira katika migodi midogo, ya kati na mikubwa. Aidha, kaguzi hizo zitahusisha mabwawa ya kuhifadhia topetaka (TSF), sehemu ya kuhifadhia miambataka (*Waste Rock Dump* - WRD) na maghala ya kuhifadhia baruti. Vilevile, Tume ya

Madini itaendelea kusimamia uwasilishaji na utekelezaji wa mipango ya uendelezaji na ufungaji migodi.

***“Serikali itaendelea kuchukua hatua stahiki kuhakikisha wachimbaji wanafuata taratibu za uchimbaji salama ili kuepuka ajali zisizo za lazima na ambazo zinaweza kuzuilika”***

**d) Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini (Local Content) na Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii (CSR)**

***189. Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia Ushirikishwaji wa watanzania katika Sekta ya Madini, Tume ya Madini itaendelea kutekeleza na kuhakikisha kuwa kampuni zinazomiliki leseni za madini zinanunua bidhaa na huduma zinazopatikana nchini.

***190. Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha Ushirikishwaji wa Watanzania kwenye Sekta ya Madini, Tume ya Madini itaendelea kutangaza orodha ya huduma na bidhaa zinazotakiwa kutolewa na kampuni zinazomilikiwa na Watanzania kwa asilimia 100. Aidha, Tume ya Madini itaendelea kusimamia wamiliki wa leseni za madini nchini kutimiza takwa la uwajibikaji kwa jamii (CSR).

***"Ni marufuku kwa mtu ambaye si Mtanzania kusambaza bidhaa au kutoa huduma zilizotangazwa kufanywa na Watanzania kwa asilimia mia moja"***

**e) Kuboresha Mazingira ya Utendaji Kazi na Kuwajengea Uwezo Watumishi**

***191. Mheshimiwa Spika,*** ili kujiimarisha katika utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Tume ya Madini imepanga kununua vitendea kazi na ujenzi wa majengo ya ofisi, ambapo itaendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi za Afisa Madini wakazi tatu (3) ambazo ni Mahenge, Rukwa na Songwe; Ukarabati wa majengo ya Ofisi za Afisa Madini Wakazi Morogoro, Mtwara na Mbeya; ununuzi wa vitendea kazi vikiwemo magari (25), kompyuta (300), pikipiki (100) na vifaa vya masoko ya madini ikijumuisha XRF 40 na mizani 20; ununuzi wa vifaa vya ukaguzi wa migodi na mazingira; pamoja na ujenzi wa mfumo wa Kanzidata ya Madini.

***192. Mheshimiwa Spika,*** Ili kuhakikisha Tume ya Madini inatekeleza majukumu yake ipasavyo, itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu (70) na muda mfupi (170) katika kada mbalimbali kwa kuzingatia uhitaji uliopo. Aidha, Tume ya Madini itajaza nafasi kwa njia ya uhamisho (2) na ajira mpya (2).

**(ii) Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)**

***193. Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, GST imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

**a) Kufanya Tafiti za Jiosayansi na Kuboresha Kanzidata ya Taifa ya Taarifa za Miamba na Madini**

***194. Mheshimiwa Spika,*** GST itafanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege na ugani wa jiolojia na jiokemia katika QDS mbili (QDS 239 na 240) zilizopo Wilaya za Rufiji na Kilwa na kuchora ramani zake. QDS hizo ni miongoni mwa QDS 11 zilizobakia nchini bila kuchorewa ramani ya jiolojia ili kukamilisha asilimia 100 ya utafiti wa jiolojia ya utambuzi wa miamba kutoka asilimia 97 ya sasa na utafiti maalumu kwa ajili ya kutambua maeneo yenye Madini Muhimu na Madini Mkakati.

***195. Mheshimiwa Spika,*** GST itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Mfumo wa Kanzidata ya Taifa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kukamilika kwa mfumo huo kutaongeza usalama wa taarifa za jiosayansi na utarahisisha uhifadhi na usambazaji wake kwa wadau. Aidha, GST itachora ramani

25, kuhariri na kudurufu ramani 30 na kuchakata picha za satelaiti kwa ajili ya kuwezesha shughuli za ugani; na kuingiza taarifa/machapisho 500 katika mfumo wa digitali.

***196. Mheshimiwa Spika,*** GST itakusanya, itahakiki na kutathmini uhalisia wa taarifa na takwimu za jiosayansi kutoka kwa wamiliki wa leseni 40 za utafutaji na uchimbaji madini nchini; kuhuisha Kanzidata ya Rasilimali Madini ya Taifa pamoja na Kitabu cha Madini Yapatikanayo Tanzania; kukusanya na kuchakata taarifa za miamba choronge mita 1,000 kutoka kwa wamiliki wa leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini.

**b) Kuwajengea Uwezo Wachimbaji Wadogo**

***197. Mheshimiwa Spika,*** katika kuwajengea uwezo wachimbaji wadogo, GST inalenga kufanya utafiti wa jiosayansi katika eneo litakalotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo kwa kutumia vifaa vya kisasa ikiwemo ndege nyuki (drone) ili kupata taarifa za kina za jiofizikia kwa lengo la kubaini sehemu zenye viashiria vya uwepo wa madini katika eneo hilo. Aidha, GST itatoa mafunzo kuhusu kutambua ulalo, mwelekeo, tabia za mbale kwa uchenjuaji katika mikoa minne (4) ambayo ni Rukwa, Katavi, Kigoma na Kagera yenye shughuli hai za uchimbaji mdogo wa madini.

### c) Kuboresha Huduma za Maabara

***198. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma za maabara, GST itaendelea kufanya uchunguzi wa sampuli mbalimbali kwa kuzingatia vigezo vya ithibati (accreditation). Aidha, GST itaendelea na ujenzi wa maabara mpya ya kisasa ya uchunguzi wa madini (State of the Art Geoscientific Laboratory) katika eneo la Kizota Dodoma. Vilevile, GST itaendelea na ujenzi wa maabara za kanda katika mikoa ya kimadini ya Chunya na Geita ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vyake kwa lengo la kusogeza karibu huduma kwa wananchi wanaojihusisha na shughuli za madini.

***199. Mheshimiwa Spika,*** GST itaendelea kutengeneza vyungu (crucibles and cupels) 250,000 kwa ajili ya kuwezesha uchunguzi wa sampuli za miamba na udongo hususani dhahabu. Aidha, GST itafanya uchunguzi wa sampuli 25,000 za udongo, miamba na madini na uandaaji wa sampuli rejea za ndani (internal certified reference materials) za dhahabu, shaba, fedha, zinki, chuma na *cobalt*.

### d) Ufuatiliaji na Kuelimisha Umma Kuhusu Majanga ya Asili ya Jiolojia

***200. Mheshimiwa Spika,*** GST itakusanya na kuchakata taarifa kutoka vituo vinne (4) vya kudumu vya kunakili mienendo ya mitetemo vilivyopo katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Geita na Mbeya. Aidha, GST itahuisha ramani inayoonesha vitovu vya matetemeko ya ardhi nchini. Sambamba, na hilo, GST itafanya matengenezo kinga ya vifaa vya kunakili mitetemo. Vilevile, GST itaendelea kutoa elimu kwa umma kwa njia ya machapisho, semina na vyombo vya habari kuhusu namna bora ya kujikinga na kupunguza athari za majanga ya asili ya jiolojia.

### e) Kuwajengea Uwezo Watumishi wa GST katika Kutekeleza Majukumu

***201. Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uwezo wa Taasisi katika kutekeleza majukumu yake, GST itaboresha mifumo ya ndani ya uchakataji, uhifadhi, usambazaji wa taarifa, takwimu za jiosayansi na taarifa za uwepo wa madini. Aidha, GST itawajengea uwezo watumishi 30 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani mbalimbali ikiwemo masuala ya maabara.

***202. Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi, GST itaendelea na taratibu za ununuzi wa

vitendea kazi ikiwemo helikopta na ndege nyuki (drone) kwa lengo la kuongeza kasi ya kufanya utafiti wa kina wa madini nchini ikiwemo maeneo ya wachimbaji wadogo. Aidha, taasisi itanunua vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa sampuli za madini mbalimbali yakiwemo ya kimkakati, kukarabati majengo, kukamilisha ujenzi wa maabara kwenye kanda, kuboresha mikakati ya ukusanyaji mapato na usimamizi wa rasilimali watu na fedha.

### (iii) Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

***203. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, STAMICO imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

#### i. Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato

***204. Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha mapato ya Shirika yanakua na kuimarika, Shirika limepanga kuongeza usimamizi kwenye uwekezaji uliopo katika miradi yake kama ifuatavyo:

#### a) Uzalishaji wa Makaa ya Mawe na Nishati Safi ya Rafiki Briquettes

***205. Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaendelea na uzalishaji wa makaa ya mawe katika eneo la Kabulo-Kiwira ambapo jumla ya tani 600,000 zimepangwa kuchimbwa.

Aidha, Shirika linatarajia kukusanya shilingi 19,397,614,979.00 kutokana na uzalishaji huo utakaofanyika. Ili kufanikisha lengo hilo, Shirika limepanga kununua mitambo na vifaa mbalimbali vikiwemo *bull-dozer D8* (1), *longwall coal shearer* (2), *chain conveyor* (8), *hydraulic prop (1), underground and pit communication* (1) na *excavator* (1).

**206. *Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaendelea na uzalishaji wa Nishati Safi ya *Rafiki Briquettes* kwa kutumia mitambo yake minne (4) ya Kisarawe, Kiwira, Chigongwe na Tabora na kuanza usimikaji wa mtambo mwingine katika Mkoa wa Geita. Kupitia mitambo hiyo, Shirika linatarajia kuzalisha jumla ya tani 25,470 za nishati safi zenye thamani ya shilingi 19,416,000,000.00.

### b) Kuimarisha Shughuli za Uchorongaji

**207. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Shirika litaendelea kuimarisha shughuli za uchorongaji kwa kutangaza huduma hizo na kutafuta kandarasi ndani na nje ya nchi pamoja na kununua mitambo mitatu (3) na vifaa vya uchorongaji. Shirika linakadiria kufanya uchorongaji wa mita 196,980 zenye thamani ya shilingi 89,823,450,000.00.

### c) Uzalishaji wa Kokoto - Chigongwe

***208. Mheshimiwa Spika*****,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Shirika limepanga kuzalisha mita za ujazo 94,400 za kokoto katika mradi wa Chigongwe. Uzalishaji huo unatarajiwa kuliingizia Shirika mapato ya shilingi 3,350,400,000.00. Aidha, katika kuhakikisha kunakuwa na soko la kokoto, Shirika limeendelea kufanya mazungumzo na kampuni mbalimbali kubwa za ujenzi katika miradi ya Serikali ikiwemo majengo, barabara, reli, viwanja vya mpira na viwanja vya ndege.

### ii. Kuwezesha Shughuli za Uchimbaji Mdogo na Kuimarisha Vituo vya Mfano

***209. Mheshimiwa Spika,*** STAMICO itaendelea kuwezesha wachimbaji wadogo kwa kufanya yafuatayo: kuendelea kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa vituo vya mfano vya Itumbi, Lwamgasa na Katente pamoja na mitambo 15 ya uchorongaji; kuendelea na uzalishaji katika mgodi wa mfano Lwamgasa; kuanza uzalishaji katika kiwanda cha chumvi kilichopo Mkoa wa Lindi; kukamilisha upanuzi wa Kituo cha mfano cha Katente; na kusimika mitambo miwili (2) ya uchenjuaji yenye uwezo wa kuchakata tani 120 za mbale ya dhahabu kwa siku kwa kila mtambo katika eneo la wachimbaji wadogo la Mwakitolyo - Shinyanga na Buhemba - Mara.

***210. Mheshimiwa Spika,*** Shirika limepanga kuzindua na kuanza kutumia mfumo wa usajili wa wachimbaji wadogo. Mfumo huu utawawezesha wachimbaji wadogo kupata taarifa za masoko, wasambazaji wa vifaa, malipo na kupata taarifa za kila siku za usajili wa wachimbaji wadogo wapya.

### iii. Kuendeleza Leseni za Madini za Shirika

***211. Mheshimiwa Spika,*** Shirika limepanga kuendelea na utafiti kwenye leseni moja (1) ya dhahabu iliyopo Wilaya ya Bukombe Mkoani Geita ambapo utafiti wake pamoja na taarifa ya upembuzi yakinifu utakamilika ifikapo Juni 2027. Vilevile, Shirika litaendelea na utafiti wa madini ya Kinywe katika leseni mbili (2) zilizopo Wilaya ya Ruangwa na Nachingwea, Mkoani Lindi pamoja na leseni tatu (3) za madini ya shaba zilizopo Katavi.

### iv. Miradi ya Ubia na Kampuni Tanzu

***212. Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaimarisha uendelezaji wa miradi ya ubia ambayo ni Mgodi wa Buckreef, Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza, Mgodi wa Uchimbaji wa Madini ya Nikeli wa Ntaka pamoja na Kampuni tanzu ya STAMIGOLD ili kuongeza ufanisi na kuwezesha ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye miradi hiyo.

**213. *Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaendelea kuiwezesha STAMIGOLD kufanya utafiti unaolenga kuongeza thamani ya matokeo ya utafiti wa awali pamoja na uhakiki wa uwepo wa mashapo katika leseni ya SML 157/2003 na PL 13075/2024 kwa lengo la kuongeza uhai wa mgodi huo.

### v. Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi

**214. *Mheshimiwa Spika,*** Shirika linatambua umuhimu wa kuwa na rasilimaliwatu pamoja na mazingira bora ya utendaji kazi. Shirika limepanga kuendelea kujaza nafasi wazi, kununua vitendea kazi na kuwaendeleza watumishi katika kada mbalimbali kwa kuzingatia uhitaji uliopo. Shirika linatarajia kujaza nafasi wazi 16 za watumishi kwa utaratibu wa uhamisho na ajira mpya. Aidha, watumishi 50 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi na wanne (4) ya muda mrefu. Vilevile, Shirika litaendelea kusimamia na kuhakikisha maslahi na stahiki za watumishi zinapatikana kwa wakati. Kadhalika, Shirika litajenga jengo la Makao Makuu lenye ghorofa 10 jijini Dodoma.

## (iv) Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)

**215. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, TGC imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

### a) Utoaji Mafunzo ya Uongezaji Thamani Madini

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** TGC itaendelea kutoa mafunzo katika programu tatu (3) kwa ngazi ya Stashahada katika teknolojia za madini ya vito na usonara; kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za utambuzi wa madini ya vito, usonara, utengenezaji wa bidhaa za mapambo na urembo zinazotokana na miamba na vito na usanifu madini ya vito; na kufanya uhamasishaji kuhusu masuala ya uongezaji thamani madini ya vito katika shule za msingi na sekondari.

### b) Uzalishaji wa Bidhaa za Madini Zilizoongezwa Thamani

**217.** ***Mheshimiwa Spika,*** TGC imepanga kuzalisha na kuuza bidhaa za usonara na ukataji wa madini ya vito 1300, bidhaa za usonara 1400, bidhaa za miamba 7200, Shanga 7500. Bidhaa hizo zinatarajiwa kuwa na thamani ya shilingi 135,000,000.00

### c) Huduma za Upimaji wa Sampuli za Madini ya Vito

**218.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuongeza ufanisi wa huduma za maabara TGC imepanga kuimarisha ufanisi wa maabara ambapo itaboresha huduma za upimaji wa madini ya vito hadi kufikia uwezo wa kupima sampuli 1200 kwa mwaka.

#### d) Utafiti wa Madini ya Vito na Metali

***219. Mheshimiwa Spika,*** TGC kwa kushirikiana na Taasisi ya Jemolojia ya Nchini Thailand (GIT) imepanga kufanya utafiti wa ubora na viwango vya madini ya Tanzanite. Tafiti hizi zitaongeza ubunifu na tija katika shughuli mbalimbali za uongezaji thamani kwa madini ya vito na metali.

#### e) Kuwajengea Uwezo Watumishi na Kuboresha Mazingira ya Kazi

***220. Mheshimiwa Spika****,* ili kuendelea kuongeza idadi ya wakufunzi waliobobea katika fani za jemolojia, usonara na ukataji na ung'arishaji madini ya vito, TGC itawawezesha watumishi saba (7) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi. Lengo ni kuendelea kuwajengea uwezo katika maeneo yao ya utekelezaji wa majukumu. Aidha, TGC imepanga kununua mashine na vifaa mbalimbali kwa ajili ya karakana za mafunzo na uchakataji madini pamoja na ununuzi wa gari moja (1).

***221. Mheshimiwa Spika,*** TGC itaendelea na usimamizi wa ujenzi wa Jengo la ghorofa 8 (Twin Tower Building). Jengo hili litakuwa na miundombinu mbalimbali ikiwemo madarasa, karakana za uongezaji thamani madini, maabara ya kisasa ya madini ya vito na bidhaa za

usonara, *mineral gallery*, ofisi, mabweni kwa ajili ya wanafunzi, kantini na maduka.

**(v) Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)**

***222. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, TEITI imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

**a) Kuandaa na Kuweka Wazi Taarifa ya 17 ya TEITI ya Mwaka wa Fedha 2024/2025**

***223. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya TEITI itaandaa na kuweka wazi taarifa ya 17 ya TEITI ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 ya ulinganishi wa malipo ya kodi na tozo kutoka kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato yaliyopokelewa na Serikali. Uandaaji wa taarifa hiyo ni utekelezaji wa vigezo vya uwazi na uwajibikaji vya mwaka 2023 ambapo nchi wanachama wa EITI hutakiwa kuandaa na kuweka wazi taarifa husika kila mwaka. Vilevile, utekelezaji wa takwa hili ni kwa mujibu wa Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Usimamizi wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia, Sura 447.

**b) Kuweka Wazi Mikataba ya Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia**

***224. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya TEITI itaendelea kuweka wazi mikataba ambayo Serikali imeingia na Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia hapa nchini ikiwa ni utekelezaji wa Sheria inayosimamia majukumu ya TEITI pamoja na utekelezaji wa Matakwa ya Kimataifa ya EITI.

**c) Kuweka Wazi Orodha ya Wamiliki wa Hisa katika Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia**

***225. Mheshimiwa Spika,*** TEITI itaendelea kuweka wazi majina ya wamiliki wa hisa katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia (Beneficial ownership disclosure) kupitia ripoti zake za kila mwaka. Aidha, TEITI inakamilisha uandaaji wa rejista ya uwekaji wa majina ya wamiliki wa hisa ikiwa ni utekelezaji wa matakwa ya Kimataifa ya Uwazi na Uwajibikaji katika rasilimali madini, mafuta na gesi asilia (EITI Standard, 2023).

**d) Kutoa Elimu kwa Umma Kuhusu Matumizi ya Takwimu Zinazotolewa Kwenye Ripoti za TEITI**

***226. Mheshimiwa Spika*****,** TEITI itaendelea kutoa elimu kwa umma kwa kuwafikia wadau ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi, kufanya warsha katika maeneo ambapo shughuli za

uchimbaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia zinatekelezwa, na kufanya vipindi vya redio na runinga ili kutangaza majukumu ya taasisi na kuhamasisha matumizi ya takwimu zinazotolewa kwenye taarifa za TEITI. Lengo ni kuongeza uelewa kwa wananchi na wadau juu ya mapato na matumizi yatokanayo na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia.

**e) Kuwajengea Uwezo Watumishi**

**227.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuhakikisha TEITI inatekeleza majukumu yake ipasavyo, itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi wanne (4) na muda mfupi 12 katika kada mbalimbali kwa kuzingatia uhitaji uliopo.

**f) Kufanya Tafiti za Namna Wananchi Wanavyonufaika na Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia**

**228.** ***Mheshimiwa Spika,*** TEITI itaendelea kufanya utafiti kuhusu utekelezaji wa sheria katika eneo la Ushirikishwaji wa Watanzania (Local Content) katika Sekta ya Uziduaji na Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (Corporate Social Responsibility - CSR) katika Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia. Aidha, TEITI itaendelea kufanya tafiti katika

Sekta ya Uziduaji ili kuishauri Serikali namna bora ya kuboresha usimamizi wa Sekta ya Uziduaji.

### g) Utekelezaji wa Vigezo vya EITI Nchini

***229. Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2023 Tanzania ilifanyiwa tathmini ya utekelezaji wa vigezo vya EITI ambapo ilipata hadhi ya daraja la *moderate* kwa kiwango cha asilimia 77. Taasisi hii ya EITI ndio taasisi yenye jukumu la Kimataifa la kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Uziduaji kwa nchi wanachama ikiwemo Tanzania. Taasisi hiyo imepanga kufanya tathmini ya nne (4) kwa TEITI Mwezi Januari, 2027. Aidha, tathmini hiyo itapima utekelezaji wa vigezo vya EITI. Ili kukamilisha tathmini hiyo, TEITI itafanya maandalizi husika.

## E. SHUKRANI

***230. Mheshimiwa Spika,*** natambua wazi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na juhudi kubwa za kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi yetu unaimarika. Kasi, juhudi na ubunifu mkubwa wa utendaji kazi anaoendelea nao **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** vinachochea kukua kwa maendeleo ya nchi yetu.

***231. Mheshimiwa Spika,*** kipekee nitumie fursa hii kumshukuru tena kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa

miongozo na maelekezo anayotupatia katika Sekta ya Madini ambayo yanaifanya sekta hii kuendelea kukua kwa kasi na kuvutia wawekezaji kwa manufaa ya Taifa.

**232.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa **Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa maelekezo na miongozo ambayo amekuwa akiitoa kwa Sekta ya Madini ili kuimarisha usimamizi na utendaji wa shughuli mbalimbali za sekta kwa manufaa ya Taifa.

**233.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia nimshukuru **Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa usimamizi wake makini wa shughuli za kila siku za Serikali.

**234.** ***Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru wadau wa Sekta ya Madini wakiwemo Chemba ya Migodi, FEMATA, TAWOMA, TAMIDA, CHAMMATA, WIMA, TWIMI, TAMISA na vyama vingine vya wachimbaji madini, watafutaji, wachimbaji, wamiliki wa mitambo ya uchenjuaji, uyeyushaji na usafishaji madini, wafanyabiashara wa madini na watoa huduma kwa kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi. Hii imerahisisha usimamizi wa Sekta ya Madini.

***235. Mheshimiwa Spika,*** nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitazishukuru taasisi za fedha hususan mabenki kwa kuendelea kuwapa mikopo wadau wa Sekta ya Madini wakiwemo wachimbaji wakubwa, wa kati na wadogo. Vilevile, nivishukuru Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kutuhakikishia usalama na kushirikiana nasi katika kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini kwenye maeneo yenye shughuli za madini bila kusahau vyombo vya habari kwa ushirikiano wanaotupatia katika kuitangaza Sekta ya Madini.

***236. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru wananchi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka migodi na watanzania wote kwa ujumla kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa wawekezaji katika maeneo yao. Hakika wamekuwa sehemu ya mafanikio ya Sekta ya Madini nchini.

## F. HITIMISHO

***237. Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli ya shilingi 1,406,006,031,000.00 naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha makadirio ya shilingi 174,983,580,000.00 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa mchanganuo ufuatao:

(i) shilingi 71,507,708,000.00 sawa na asilimia 40.87 ya bajeti yote ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

(ii) shilingi 103,475,872,000.00 sawa na asilimia 59.13 ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 27,365,095,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi (PE) na shilingi 76,110,777,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ya Wizara na Taasisi zake.

***238. Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Majedwali na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu Sekta ya Madini vimeambatishwa pamoja na hotuba hii. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Madini kwa kikoa cha *https://www.madini.go.tz.*

***239. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**VIAMBATISHO**

**Jedwali Na. 1:** *Makusanyo Halisi ya Maduhuli kwa Kila Ofisi ya RMO Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Pamoja na Makadirio Kwa Mwaka 2026/2027*

| Na. | Kituo cha Makusanyo | Lengo la Makusanyo 2025/2026 | Lengo la Makusanyo (Julai, 2025 - Machi,2026) | Makusanyo Halisi (Julai, 2025 -Machi, 2026) | Asilimia ya Makusanyo | Lengo la Makusanyo kwa Mwaka 2026/2027 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Singida | 30,000,000,000.00 | 22,500,000,000.00 | 33,566,708,693.91 | 149.19 | 45,000,000,000.00 |
| 2 | Mwanza | 12,000,000,000.00 | 9,000,000,000.00 | 13,014,686,911.34 | 144.61 | 16,000,000,000.00 |
| 3 | Geita | 27,000,000,000.00 | 245,250,000,000.00 | 334,621,903,037.86 | 136.44 | 400,000,000,000.00 |
| 4 | Shinyanga | 32,000,000,000.00 | 24,000,000,000.00 | 32,177,206,072.88 | 134.07 | 42,000,000,000.00 |
| 5 | Mbeya | 4,600,000,000.00 | 3,450,000,000.00 | 4,470,405,394.80 | 129.58 | 6,000,000,000.00 |
| 6 | Tanga | 11,000,000,000.00 | 8,250,000,000.00 | 10,623,113,642.29 | 128.77 | 14,000,000,000.00 |
| 7 | Katavi | 10,000,000,000.00 | 7,500,000,000.00 | 9,506,757,631.94 | 126.76 | 15,000,000,000.00 |
| 8 | Kagera | 7,200,000,000.00 | 5,400,000,000.00 | 6,772,719,891.08 | 125.42 | 10,000,000,000.00 |
| 9 | Chunya | 72,000,000,000.00 | 54,000,000,000.00 | 66,337,392,771.37 | 122.85 | 87,000,000,000.00 |
| 10 | Tabora | 13,000,000,000.00 | 9,750,000,000.00 | 11,235,049,940.25 | 115.23 | 16,000,000,000.00 |
| 11 | Dar es Salaam | 24,000,000,000.00 | 18,000,000,000.00 | 20,652,007,337.67 | 114.73 | 33,000,000,000.00 |
| 12 | Mbogwe | 51,000,000,000.00 | 38,250,000,000.00 | 42,180,234,411.91 | 110.28 | 64,000,000,000.00 |
| 13 | Kigoma | 1,900,000,000.00 | 1,425,000,000.00 | 1,553,048,694.01 | 108.99 | 2,500,000,000.00 |
| 14 | Kahama | 166,000,000,000.00 | 124,500,000,000.00 | 135,500,262,365.53 | 108.84 | 176,000,000,000.00 |
| 15 | Manyara | 2,200,000,000.00 | 1,650,000,000.00 | 1,753,449,812.13 | 106.27 | 2,700,000,000.00 |
| 16 | Mara | 210,000,000,000.00 | 157,500,000,000.00 | 166,407,183,240.53 | 105.66 | 220,000,000,000.00 |
| 17 | Kilimanjaro | 4,200,000,000.00 | 3,150,000,000.00 | 3,119,743,352.02 | 99.04 | 5,000,000,000.00 |
| 18 | Lindi | 10,500,000,000.00 | 7,875,000,000.00 | 7,788,281,022.65 | 98.90 | 15,000,000,000.00 |
| 19 | Iringa | 1,400,000,000.00 | 1,050,000,000.00 | 1,011,446,730.79 | 96.33 | 1,600,000,000.00 |
| 20 | Simiyu | 4,760,000,000.00 | 3,570,000,000.00 | 3,431,455,359.38 | 96.12 | 6,000,000,000.00 |
| 21 | Songwe | 70,000,000,000.00 | 52,500,000,000.00 | 49,801,081,504.23 | 94.86 | 81,000,000,000.00 |
| 22 | Arusha | 6,700,000,000.00 | 5,025,000,000.00 | 4,421,463,237.08 | 87.99 | 7,000,000,000.00 |
| 23 | Ruvuma | 39,000,000,000.00 | 29,250,000,000.00 | 25,174,206,310.91 | 86.07 | 40,000,000,000.00 |
| 24 | Makao Makuu | 47,859,405,500.00 | 35,894,554,125.00 | 30,068,372,131.04 | 83.77 | 52,204,031,000.00 |
| 25 | Mirelani | 6,000,000,000.00 | 4,500,000,000.00 | 3,704,927,202.15 | 82.33 | 6,500,000,000.00 |
| 26 | Mahenge | 1,300,000,000.00 | 975,000,000.00 | 707,790,446.20 | 72.59 | 1,400,000,000.00 |
| 27 | Dodoma | 9,000,000,000.00 | 6,750,000,000.00 | 4,731,373,522.28 | 70.09 | 12,000,000,000.00 |
| 28 | Maabara | 828,594,500.00 | 621,445,875.00 | 416,516,000.00 | 67.02 | 900,000,000.00 |
| 29 | Morogoro | 6,500,000,000.00 | 4,875,000,000.00 | 3,118,660,743.52 | 63.97 | 8,000,000,000.00 |
| 30 | Mtwara | 11,900,000,000.00 | 8,925,000,000.00 | 4,750,198,458.32 | 53.22 | 13,500,000,000.00 |

| Na. | Kituo cha Makusanyo | Lengo la Makusanyo 2025/2026 | Lengo la Makusanyo (Julai, 2025 - Machi,2026) | Makusanyo Halisi (Julai, 2025 -Machi, 2026) | Asilimia ya Makusanyo | Lengo la Makusanyo kwa Mwaka 2026/2027 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 31 | Njombe | 5,000,000,000.00 | 3,750,000,000.00 | 1,517,290,618.92 | 40.46 | 5,500,000,000.00 |
| 32 | Rukwa | 1,150,000,000.00 | 862,500,000.00 | 318,961,431.10 | 36.98 | 1,200,000,000.00 |
| **Jumla (Shilingi)** | | **1,199,998,000,000.00** | **899,998,500,000.00** | **1,034,453,897,920.09** | **114.94** | **1,406,004,031,000.00** |

***Chanzo:*** *Tume ya Madini, Machi 2026*

***Jedwali Na. 2:*** *Kiasi cha Mrabaha na Ada ya Ukaguzi Kilichokusanywa Kutoka Kwenye Mauzo ya Madini Mbalimbali Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026*

| Na. | Aina ya Madini | Kizio | Uzito | Thamani | Mrabaha | Ada ya ukaguzi | Jumla ya Mrabaha & Ada ya ukaguzi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Dhahabu (Wachimbaji wakubwa) | Kilogramu | 28,248 | 7,158,188,594,598 | 390,878,969,531 | 54,040,438,032 | 444,919,407,563 | 46.47 |
| 2 | Dhahabu (Wachimbaji wa kati) | Kilogramu | 6,112 | 1,186,433,485,701 | 58,865,371,405 | 6,548,607,646 | 65,413,979,051 | 6.83 |
| 3 | Dhahabu (Wachimbaji wadogo) | Kilogramu | 17,459 | 5,174,378,491,211 | 275,366,948,978 | 36,281,098,386 | 311,648,047,365 | 32.55 |
| 4 | Madini ya Dhahabu | Tani | 2,733 | 30,474,464,460 | 1,906,750,350 | 317,791,740 | 2,224,542,090 | 0.23 |
| 5 | Madini ya Shaba | Tani | 28,003 | 714,244,418,878 | 42,431,399,677 | 7,051,726,166 | 49,483,125,843 | 5.17 |
| 6 | Fedha (Ag) | Kilogramu | 522.36585 | 2,725,876,408 | 166,646,832 | 27,927,769 | 194,574,601 | 0.02 |
| 7 | Bati | Tani | 304.1231 | 21,079,917,300 | 1,251,695,286 | 208,612,194 | 1,460,307,481 | 0.15 |
| 8 | Almasi | Karati | 294,865 | 109,315,499,461 | 6,437,028,228 | 1,072,838,046 | 7,509,866,274 | 0.78 |
| 9 | Tanzanite (iliyokatwa na kusanifiwa) | Karati | 9,468 | 5,059,807,336 | 52,570,441 | 51,474,384 | 104,044,825 | 0.01 |
| 10 | Tanzanite (Ghafi) | Kilogramu | 21,995 | 7,466,884,402 | 448,013,064 | 74,668,844 | 522,681,908 | 0.05 |
| 11 | Tanzanite (Magonga) | Kilogramu | 65,961 | 309,319,311 | 18,559,159 | 3,093,193 | 21,652,352 | 0.00 |
| 12 | Kinywe | Tani | 81,520 | 99,144,680,841 | 2,980,032,767 | 873,022,186 | 3,853,054,953 | 0.40 |
| 13 | Makaa ya mawe | Tani | 2,201,441 | 699,950,878,624 | 15,228,292,224 | 6,267,102,052 | 21,495,394,276 | 2.25 |
| 14 | Madini mengine ya vito ghafi | Tani | 18,205 | 37,004,164,375 | 2,099,518,409 | 374,863,400 | 2,474,381,808 | 0.26 |
| 15 | Madini mengine ya vito Iliyokatwa na kusanifiwa | Karati | 154,003 | 43,814,777,803 | 449,943,656 | 435,346,683 | 885,290,338 | 0.09 |
| 16 | Madini mengine ya Metali | Tani | 92,677 | 55,694,736,812 | 5,240,623,749 | 863,312,152 | 6,103,935,902 | 0.64 |
| 17 | Madini mengine ya viwandani | Tani | 12,269,218 | 364,041,807,755 | 10,608,872,838 | 3,520,077,829 | 14,128,950,668 | 1.48 |
| 18 | Madini Ujenzi | Tani | 30,215,970 | 535,707,335,599 | 16,428,371,707 | 5,471,572,545 | 21,899,944,252 | 2.29 |
| 19 | Sampuli za Madini | Kilogramu | 7,827 | 402,358,267 | 25,885,579 | 4,433,746 | 30,319,325 | 0.00 |
| 20 | Other minerals | | | | 4,304,747,967 | -1,282,217,772 | 3,022,530,195 | 0.32 |

| Na. | Aina ya Madini | Kizio | Uzito | Thamani | Mrabaha | Ada ya ukaguzi | Jumla ya Mrabaha & Ada ya ukaguzi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla (Shilingi) | | | 16,245,437,499,141.10 | 835,190,241,847.76 | 122,205,789,221.86 | 957,396,031,069.62 | 1.00 |

***Chanzo:*** *Tume ya Madini, Machi 2026*

**Jedwali Na. 3:** *Mwenendo wa Mauzo na Mapato ya Dhahabu Katika Masoko ya Geita, Kahama na Chunya kwa Kipindi cha Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026*

| SOKO LA CHUNYA | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Mwezi | Uzito (g) | Thamani | Mrabaha | Ada ya Ukaguzi | Jumla ya Makusanyo |
| Julai, 2025 | 349,453.65 | 76,363,752,037.62 | 4,276,370,114.11 | 610,910,016.30 | 4,887,280,130.41 |
| Agosti, 2025 | 280,510.20 | 65,989,525,441.68 | 3,695,413,424.73 | 527,916,203.53 | 4,223,329,628.27 |
| Septemba, 2025 | 342,110.92 | 82,735,236,200.59 | 4,633,173,227.23 | 661,881,889.60 | 5,295,055,116.84 |
| Oktoba, 2025 | 336,262.12 | 96,051,516,129.59 | 5,378,884,903.26 | 768,412,129.04 | 6,147,297,032.29 |
| Novemba, 2025 | 407,285.70 | 94,502,102,431.68 | 5,292,117,736.17 | 756,016,819.45 | 6,048,134,555.63 |
| Desemba, 2025 | 345,936.14 | 104,816,217,012.35 | 5,869,708,152.69 | 838,529,736.10 | 6,708,237,888.79 |
| Januari, 2026 | 345,936.14 | 104,816,217,012.35 | 5,869,708,152.69 | 838,529,736.10 | 6,708,237,888.79 |
| Februari, 2026 | 363,842.54 | 135,204,033,572.59 | 7,024,337,040.61 | 813,240,555.38 | 7,837,577,595.99 |
| Machi, 2026 | 298,533.47 | 108,546,013,107.51 | 5,763,641,380.75 | 710,900,428.22 | 6,474,541,808.97 |
| **Jumla (Shilingi)** | **3,069,870.88** | **869,024,612,945.96** | **47,803,354,132.25** | **6,526,337,513.72** | **54,329,691,645.97** |
| | | | | | |
| SOKO LA GEITA | | | | | |
| Mwezi | Uzito (g) | Thamani | Mrabaha | Ada ya Ukaguzi | Jumla ya Makusanyo |
| Julai, 2025 | 245,309.33 | 62,197,277,369.90 | 3,483,047,532.71 | 497,578,218.96 | 3,980,625,751.67 |
| Agosti, 2025 | 235,062.83 | 57,289,770,656.59 | 3,208,227,156.77 | 458,318,165.25 | 3,666,545,322.02 |
| Septemba, 2025 | 286,750.60 | 74,117,426,166.27 | 4,150,575,865.31 | 592,939,409.33 | 4,743,515,274.64 |
| Oktoba, 2025 | 253,073.31 | 73,465,736,359.61 | 4,114,081,236.14 | 587,725,890.88 | 4,701,807,127.02 |
| Novemba, 2025 | 256,536.70 | 75,129,517,754.92 | 4,207,396,126.79 | 601,036,142.04 | 4,808,432,268.83 |
| Desemba, 2025 | 240,541.85 | 73,726,511,827.04 | 4,128,684,662.31 | 589,812,094.62 | 4,718,496,756.93 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Januari, 2026 | 308,742.67 | 104,979,836,166.07 | 5,456,684,325.55 | 628,745,439.45 | 6,085,429,765.00 |
| Februari, 2026 | 234,098.78 | 88,157,423,393.60 | 5,589,237,840.33 | 814,011,010.78 | 6,403,248,851.11 |
| Machi, 2026 | 183,309.29 | 67,064,293,161.14 | 3,755,600,417.02 | 536,514,345.29 | 4,292,114,762.31 |
| **Jumla (Shilingi)** | **2,243,425.37** | **676,127,792,855.15** | **38,093,535,162.94** | **5,306,680,716.60** | **43,400,215,879.54** |
| | | | | | |
| **SOKO LA KAHAMA** | | | | | |
| **Mwezi** | **Uzito (g)** | **Thamani** | **Mrabaha** | **Ada ya Ukaguzi** | **Jumla ya Makusanyo** |
| Julai, 2025 | 141,326.49 | 36,250,481,384.94 | 1,950,848,404.41 | 250,414,574.51 | 2,201,262,978.92 |
| Agosti, 2025 | 209,987.98 | 51,267,011,751.19 | 2,746,354,257.63 | 349,654,014.43 | 3,096,008,272.05 |
| Septemba, 2025 | 181,207.88 | 48,640,895,877.05 | 2,582,392,905.44 | 318,378,535.18 | 2,900,771,440.61 |
| Oktoba, 2025 | 221,058.44 | 66,654,493,166.18 | 3,561,232,369.78 | 447,526,321.56 | 4,008,758,691.34 |
| Novemba, 2025 | 213,871.56 | 63,487,512,705.01 | 3,067,454,548.73 | 263,977,020.26 | 3,331,431,568.99 |
| Desemba, 2025 | 211,387.97 | 66,178,167,473.88 | 3,170,360,924.63 | 261,617,112.83 | 3,431,978,037.46 |
| Januari, 2026 | 132,436.90 | 41,277,275,377.00 | 2,477,754,827.03 | 461,010,019.80 | 2,938,764,846.83 |
| Februari, 2026 | 135,565.82 | 48,577,676,447.65 | 3,044,660,586.82 | 485,430,688.75 | 3,530,091,275.57 |
| Machi, 2026 | 195,997.24 | 74,215,776,566.77 | 3,630,953,854.21 | 450,732,470.73 | 4,081,686,324.94 |
| **Jumla (Shilingi)** | **1,642,840.28** | **496,549,290,749.67** | **26,232,012,678.67** | **3,288,740,758.06** | **29,520,753,436.72** |

***Chanzo:*** *Tume ya Madini, Machi 2026*

***Jedwali Na. 4:*** *Mapato Yaliyotokana na Mauzo ya Madini Kwenye Masoko ya Madini Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026*

| Na. | Jina la Soko | Aina ya Madini | Kizio | Uzito | Thamani | Mrabaha | Ada ya Ukaguzi | Jumla ya Makusanyo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | Gold | Gram | 15,261.08 | 5,052,901,043.27 | 277,569,968.85 | 35,195,472.23 | 312,765,441.08 |
| 2 | Arusha | Gemstone | Carat | 148,917.65 | 40,934,164,005.28 | 410,165,082.36 | 410,078,673.65 | 820,243,756.01 |
| 3 | Arusha | Gemstone | Gram | 8,442,434,417.41 | 12,424,102,715.15 | 743,913,043.48 | 124,241,101.47 | 868,154,144.95 |
| 4 | Babati | Gold | Gram | 6,937.61 | 2,169,481,795.12 | 106,306,657.52 | 1,294,744.69 | 107,601,402.21 |
| 5 | Chunya | Gold | Gram | 3,069,870.88 | 869,024,612,945.96 | 47,803,354,132.25 | 6,526,337,513.72 | 54,329,691,645.97 |
| 6 | Dar es Salaam | Gold | Gram | 28,935.24 | 8,527,283,863.45 | 451,581,315.47 | 58,026,261.63 | 509,607,577.10 |
| 7 | Dar es Salaam | Gemstone | Carat | 190.14 | 89,780,927.11 | 930,922.34 | 897,809.27 | 1,828,731.61 |

| Na. | Jina la Soko | Aina ya Madini | Kizio | Uzito | Thamani | Mrabaha | Ada ya Ukaguzi | Jumla ya Makusanyo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 8 | Dar es Salaam | Gemstone | Gram | 287.10 | 112,835.04 | 6,770.10 | 1,128.35 | 7,898.45 |
| 9 | Dar es Salaam | Tanzanite | Carat | 5,302.33 | 2,744,154,637.74 | 28,246,078.28 | 27,549,442.04 | 55,795,520.32 |
| 10 | Dodoma | Gold | Gram | 96,079.12 | 27,415,222,310.94 | 1,196,191,164.54 | 49,876,001.70 | 1,246,067,166.24 |
| 11 | Dodoma | Gemstone | Gram | 463,318,780.96 | 1,459,542,082.30 | 87,572,524.94 | 14,595,420.82 | 102,167,945.76 |
| 12 | Geita | Gold | Gram | 2,243,425.37 | 676,127,792,855.15 | 38,093,535,162.94 | 5,306,680,716.60 | 43,400,215,879.54 |
| 13 | Hanan'g | Gold | Gram | 1,527.92 | 409,782,271.73 | 20,511,848.85 | 2,060,279.00 | 22,572,127.85 |
| 14 | Handeni | Gold | Gram | 17,028.34 | 5,524,891,207.12 | 295,939,084.47 | 42,018,152.68 | 337,957,237.15 |
| 15 | Handeni | Gemstone | Gram | 15,868.24 | 4,552,744,277.39 | 271,318,442.34 | 44,594,435.56 | 315,912,877.90 |
| 16 | Iringa | Gold | Gram | 327,224.45 | 96,793,429,516.20 | 5,426,222,719.75 | 777,981,408.81 | 6,204,204,128.55 |
| 17 | Kahama | Gold | Gram | 1,642,840.28 | 496,549,290,749.67 | 26,232,012,678.67 | 3,288,740,758.06 | 29,520,753,436.72 |
| 18 | Kakonko | Gold | Gram | 39,286.83 | 11,851,129,354.81 | 599,241,876.53 | 61,880,749.54 | 661,122,626.07 |
| 19 | Katavi | Gold | Gram | 103,485.72 | 29,725,964,584.17 | 1,524,213,679.96 | 156,602,294.81 | 1,680,815,974.77 |
| 20 | Kigoma | Gold | Gram | 73.70 | 21,232,349.59 | 1,189,011.58 | 169,858.80 | 1,358,870.38 |
| 21 | Kilindi | Gold | Gram | 92,309.81 | 29,981,964,139.99 | 1,211,619,756.88 | 6,170,595.64 | 1,217,790,352.52 |
| 22 | Kyerwa | Tin | Kilogram | 310,261.21 | 20,142,765,429.49 | 1,195,441,541.27 | 199,240,264.37 | 1,394,681,805.64 |
| 23 | Lindi | Gold | Gram | 161,979.12 | 54,112,436,895.79 | 3,030,511,418.58 | 432,935,320.57 | 3,463,446,739.15 |
| 24 | Lindi | Gemstone | Gram | 975,720.65 | 1,189,241,340.28 | 71,354,480.42 | 12,681,151.57 | 84,035,631.99 |
| 25 | Mahenge | Gemstone | Gram | 452,433.87 | 2,774,133,644.22 | 165,610,018.62 | 29,232,866.54 | 194,842,885.16 |
| 26 | Mara | Gold | Gram | 1,540,325.26 | 467,754,056,021.22 | 25,022,277,595.92 | 3,156,057,677.53 | 28,178,335,273.45 |
| 27 | Mbeya | Gold | Gram | 76,470.03 | 22,703,394,991.45 | 1,271,390,119.52 | 181,627,159.93 | 1,453,017,279.45 |
| 28 | Mbogwe | Gold | Gram | 1,245,398.20 | 417,538,128,161.37 | 22,219,135,019.47 | 3,194,044,061.74 | 25,413,179,081.20 |
| 29 | Mbulu | Gold | Gram | 28,642.63 | 8,522,032,618.71 | 395,903,505.71 | 29,389,105.22 | 425,292,610.93 |
| 30 | Mirerani | Tanzanite | Gram | 9,490,004.08 | 2,814,878,653.39 | 168,892,719.23 | 28,148,786.58 | 197,041,505.81 |
| 31 | Mirerani | Tanzanite | Carat | 3,257.47 | 788,119,508.27 | 7,881,195.08 | 7,881,195.08 | 15,762,390.16 |
| 32 | Mirerani | Gemstone | Gram | 324,384,740.60 | 964,391,316.94 | 57,863,479.01 | 9,643,913.19 | 67,507,392.20 |
| 33 | Mirerani | Gemstone | Carat | 108.07 | 1,692,108.46 | 16,921.09 | 16,921.09 | 33,842.18 |
| 34 | Morogoro | Gold | Gram | 37,126.28 | 11,745,214,479.87 | 730,851,384.40 | 64,703,950.63 | 795,555,335.03 |
| 35 | Morogoro | Gemstone | Gram | 9,445,474,755.34 | 8,251,328,168.09 | 445,025,529.88 | 70,410,171.40 | 515,435,701.28 |
| 36 | Mtwara | Gold | Gram | 18,768.81 | 5,798,467,334.46 | 332,049,853.47 | 55,024,835.85 | 387,074,689.32 |
| 37 | Mwanza | Gold | Gram | 461,324.37 | 138,595,129,994.99 | 7,210,025,305.12 | 947,015,537.95 | 8,157,040,843.07 |
| 38 | Njombe | Gold | Gram | 9,247.52 | 2,833,383,106.66 | 159,229,204.03 | 22,747,029.15 | 181,976,233.17 |
| 39 | Nyang'wale | Gold | Gram | 180,431.72 | 72,757,705,058.96 | 4,000,777,169.84 | 545,234,483.74 | 4,546,011,653.58 |
| 40 | Nyakanazi | Gold | Gram | 74,953.97 | 20,981,453,326.01 | 1,168,516,651.81 | 92,021,452.77 | 1,260,538,104.57 |
| 41 | Ruvuma | Gold | Gram | 48,087.59 | 15,014,383,650.40 | 803,298,734.89 | 100,369,932.66 | 903,668,667.55 |
| 42 | Tunduru | Gemstone | Gram | 807,515,655.74 | 4,182,044,910.28 | 250,922,694.62 | 41,506,543.38 | 292,429,237.99 |

| Na. | Jina la Soko | Aina ya Madini | Kizio | Uzito | Thamani | Mrabaha | Ada ya Ukaguzi | Jumla ya Makusanyo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 43 | Tunduru | Gold | Gram | 1,966.96 | 748,063,815.08 | 39,896,788.32 | 5,978,879.64 | 45,875,667.96 |
| 44 | Shelui | Gold | Gram | 122,632.46 | 33,272,194,901.75 | 1,985,358,823.12 | 327,235,513.66 | 2,312,594,336.78 |
| 45 | Shinyanga | Gold | Gram | 1,579,713.66 | 498,311,149,511.87 | 24,744,912,155.23 | 2,067,945,798.33 | 26,812,857,953.56 |
| 46 | Shinyanga | Diamond | Carat | 51,674.63 | 7,927,047,706.30 | 475,622,862.38 | 79,270,477.06 | 554,893,339.44 |
| 47 | Simiyu | Gold | Gram | 100,696.01 | 27,396,664,296.43 | 1,336,132,567.65 | 132,821,537.82 | 1,468,954,105.47 |
| 48 | Singida | Gold | Gram | 399,602.19 | 122,953,487,663.41 | 7,127,866,244.27 | 1,104,863,369.17 | 8,232,729,613.44 |
| 49 | Songwe | Gold | Gram | 1,243,909.34 | 376,398,438,577.74 | 19,217,712,809.87 | 2,080,891,669.14 | 21,298,604,479.01 |
| 50 | Tabora | Gold | Gram | 800,244.10 | 232,747,583,090.65 | 11,085,185,203.34 | 887,174,065.37 | 11,972,359,268.71 |
| 51 | Tanga | Gold | Gram | 6,442.07 | 2,194,347,229.28 | 89,016,262.97 | 621,186.90 | 89,637,449.87 |
| 52 | Tanga | Gemstone | Gram | 305,042,616.76 | 684,415,908.05 | 44,163,143.30 | 6,510,082.06 | 50,673,225.36 |
| **Jumla (Shilingi)** | | | | **19,815,447,240.87** | **4,903,477,353,887.03** | **259,634,483,324.52** | **32,848,237,759.15** | **292,482,721,083.67** |

***Chanzo:*** *Tume ya Madini, Machi 2026*

***Jedwali Na. 5****: Mapato Yaliyotokana na Mauzo ya Madini Kwenye Masoko ya Madini Kwa Kila Aina ya Madini Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026*

| Aina ya Madini | Kizio | Uzito | Thamani | Mrabaha | Ada ya Ukaguzi | Jumla ya Mapato |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Dhahabu | Gramu | 15,822,248.63 | 4,799,804,021,881.35 | 255,209,535,875.78 | 31,741,737,375.67 | 286,951,273,251.46 |
| Bati | Kilogramu | 310,261.21 | 20,142,765,429.49 | 1,195,441,541.27 | 199,240,264.37 | 1,394,681,805.64 |
| Almasi | Karati | 51,674.63 | 7,927,047,706.30 | 475,622,862.38 | 79,270,477.06 | 554,893,339.44 |
| Tanzanite | Karati | 8,559.80 | 3,532,274,146.01 | 36,127,273.36 | 35,430,637.12 | 71,557,910.48 |
| Tanzanite | Gramu | 9,490,004.08 | 2,814,878,653.39 | 168,892,719.23 | 28,148,786.58 | 197,041,505.81 |
| Vito | Karati | 149,215.86 | 41,025,637,040.85 | 411,112,925.79 | 410,993,404.01 | 822,106,329.80 |
| Vito | Gramu | 19,789,615,276.66 | 36,482,057,197.73 | 2,137,750,126.71 | 353,416,814.33 | 2,491,166,941.04 |
| **Jumla (Shilingi)** | | | **4,911,728,682,055.12** | **259,634,483,324.52** | **32,848,237,759.15** | **292,482,721,083.67** |

***Chanzo:*** *Tume ya Madini, Machi 2026*

***Jedwali Na. 6:*** *Mapato Yaliyotokana na Mauzo ya Madini Kwenye Masoko ya Madini Tangu Kuanzishwa Kwake Machi, 2019 hadi Machi, 2026*

| Aina ya Madini | Kizio | Uzito | Thamani | Mrabaha | Ada ya Ukaguzi | Jumla ya Mapato |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Dhahabu | Gramu | 120,057,730.96 | 19,224,134,298,139.30 | 1,102,580,350,354.37 | 172,132,250,324.43 | 1,274,712,600,678.79 |
| Bati | Kilogramu | 2,183,847.83 | 111,456,092,617.70 | 6,716,479,792.21 | 1,143,675,161.32 | 7,860,154,953.53 |
| Almasi | Karati | 151,159.47 | 49,556,367,688.15 | 2,974,236,179.71 | 496,417,795.30 | 3,470,653,975.01 |
| Tanzanite | Karati | 441,704.11 | 115,540,109,798.51 | 1,164,404,864.02 | 1,164,404,864.02 | 2,328,809,728.05 |
| Tanzanite | Gramu | 445,605,061.03 | 73,168,130,228.08 | 4,375,008,471.69 | 716,601,960.29 | 5,091,610,431.98 |
| Vito | Karati | 638,236.94 | 146,007,787,527.29 | 1,721,997,556.80 | 1,721,997,556.80 | 3,443,995,113.60 |
| Vito | Gramu | 183,272,801,071.63 | 156,392,420,787.38 | 12,905,275,880.47 | 5,085,654,841.10 | 17,990,930,721.57 |
| **Jumla (Shilingi)** | | | **19,876,255,206,786.40** | **1,132,437,753,099.27** | **182,461,002,503.26** | **1,314,898,755,602.53** |

***Chanzo:*** *Tume ya Madini, Machi 2026*

***Jedwali Na. 7:*** *Makusanyo ya Maduhuli Yaliyotokana na Vyanzo Mbalimbali Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026*

| Na. | Chanzo | Malengo 2025/2026 | Makusanyo Halisi (Julai, 2025 - Machi, 2026) | Asilimia ya Makusanyo | Lengo la Makusanyo kwa Mwaka 2026/2027 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Marejesho ya Fedha za Serikali | 2,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | 2,000,000.00 |
| 2. | Ada ya Mwaka ya leseni | 65,180,847,813.00 | 44,593,027,554.47 | 68.41 | 69,743,507,180.79 |
| 3. | Ada ya Ukaguzi | 164,263,722,901.00 | 123,115,191,215.10 | 74.95 | 192,905,922,216.17 |
| 4. | Ada za Kijiolojia | 17,131,607,188.00 | 11,967,426,987.08 | 69.86 | 18,330,819,691.03 |
| 5. | Mrabaha | 950,262,641,687.00 | 835,444,957,292.25 | 87.92 | 1,119,643,458,872.69 |
| 6. | Adhabu na Tozo | 2,534,180,411.00 | 3,724,271,868.84 | 148.43 | 4,711,573,039.32 |
| 7. | Malipo ya Huduma za Maabara | 625,000,000.00 | 416,516,000.00 | 64.08 | 668,750,000.00 |
| 8. | *HIV Response Levy* | 0.00 | 15,192,507,002.35 | 0.00 | 0.00 |
| **Jumla (Shilingi)** | | **1,200,000,000,000.00** | **1,034,453,897,920.09** | **86.20** | **1,406,006,031,000.00** |

***Chanzo:*** *Tume ya Madini, Machi 2026*

***Jedwali Na. 8:*** *Migodi ya Uchimbaji wa Kati na Mkubwa wa Madini iliyokaguliwa Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026*

| NA. | MGODI | MKOA WA KIMADINI |
|---|---|---|
| | **Migodi ya Uchimbaji wa Kati wa Madini** | |
| 1. | African Modern Mining Company | Tanga |
| 2. | Busolwa Mining Ltd | Mwanza |
| 3. | Canuck Company Limited & | Kahama. |
| 4. | CDICD Group Limited; | Dodoma |
| 5. | CGI Contractors Limited | Morogoro |
| 6. | Chongyuan Huijin (Tanzania) Co. Ltd | Geita |
| 7. | Franone Mining & Gems Co. Ltd | Mererani. |
| 8. | Igurubi Resources Limited | Tabora |
| 9. | Isinka Federation Co-operative Society | Mwanza |
| 10. | Katavi Mining Company Limited | Katavi |
| 11. | Long Fortune Pvt Limited | Kahama. |
| 12. | Mara Mine Development Ltd | Mara |
| 13. | Market Insight Limited | Njombe |
| 14. | Matongo Gold Mine | Mara |
| 15. | Maweni limestone ltd | Tanga |

| NA. | MGODI | MKOA WA KIMADINI |
|---|---|---|
| 16. | Mbeya Cement Company Limited | Mbeya |
| 17. | MMC Mining Limited | Morogoro |
| 18. | MMG Gold Limited | Mara |
| 19. | Nyati Mineral sand Limited (Fungoni Project) | Dar es salaam |
| 20. | Permanent Minerals | Mererani. |
| 21. | PolyDhahabu Mining Company Limited, | Mara |
| 22. | Pubo Mining Company LTD | Singida |
| 23. | Rz Union Mining Company Limited | Geita |
| 24. | Saniniu K. LAIZER | Mererani. |
| 25. | Tancoal Energy Limited | Ruvuma |
| 26. | Tanga Cement Ltd | Tanga |
| 27. | Tanzanite Africa & J.S Magezi Sons Limited | Mererani. |
| 28. | Tianpin (T) Investment Management Limited. | Kahama. |
| 29. | TOL Gases Limited | Mbeya |
| 30. | Tribble Seven Mining LTD | Singida |
| 31. | YUDI Mining Tanzania Graphite Company Limited | Morogoro |
| **Migodi ya Uchimbaji Mkubwa wa Madini** | | |
| 1. | Bulyanhulu Gold Mine | Kahama |


| NA. | MGODI | MKOA WA KIMADINI |
|---|---|---|
| 2. | Geita Gold Mine | Geita |
| 3. | North Mara Gold Mine | Mara |
| 4. | Nyati Mineral Sand Limited | Tanga |
| 5. | Sotta Mining Corporation | Geita |
| 6. | Williamson Diamonds Limited | Shinyanga |

***Chanzo:*** *Tume ya Madini, Machi 2026*


***Jedwali Na. 9:*** *Matukio ya Matetemeko Makubwa ya Ardhi yaliyotokea nchini Tanzania katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026*

| Na. | Tarehe | Muda (Saa 24) | Latitudo | Longitudo | Kina (km) | Ukubwa (Richter) | Mkoa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 10/07/2025 | 01:12:58 | -4.5280 | 35.1204 | 25 | 5.0 | Manyara |
| 2. | 30/07/2025 | 18:03:58 | -4.3852 | 35.1531 | 10 | 4.6 | Manyara |
| 3. | 08/08/2025 | 10:38:24 | -5.0213 | 35.0873 | 10 | 5.0 | Singida |
| 4. | 29/12/2025 | 12:51:41 | -5.3127 | 34.9465 | 10 | 4.6 | Singida |
| 5. | 29/12/2025 | 03:02:27 | -5.4216 | 34.9942 | 17 | 4.3 | Singida |
| 6. | 30/12/2025 | 04:31:57 | -4.7938 | 34.9508 | 10 | 4.2 | Singida |

***Chanzo:*** *GST, Machi 2026*




**Kielelezo Na. 1:** *Makusanyo ya Maduhuli Kutokana na Mauzo ya Dhahabu Katika Masoko Makubwa Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026*




**Kielelezo Na. 2:** *Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli Kuanzia Mwaka 2021/2022 hadi 2024/2025*



**Mtambo wa kusindika na kuyeyusha Madini ya Nikeli na Shaba uliosimikwa katika Kiwanda cha Zhong Zhou Mining kilichopo Zamahero, Wilaya ya Bahi Mkoani Dodoma.**


STATE MINING CORPORATION
(STAMICO)